# UHAKIKI WA USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA YA

# *KIJIBA CHA MOYO* NA *MSTAHIKI MEYA*

**NA**

**BIASHA SALIM KHAMIS**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi**

**Novemba 2015**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Biasha Salim Khamis | Tarehe

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Dkt. Evans Mbuthia | Tarehe

(Msimamizi)

Bw. Samson Ongarora | Tarehe

(Msimamizi)

# TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu, bwana Salim Khamis na bibi Mwanajuma Salim na mwanangu mpendwa Rehema Kwamboka kwa kunipa ari ya kupambana na masomo.

# SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kung'ang'ana na kukamilisha kazi hii. Pia nawashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kufanikisha kazi hii.

Nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt. Evans Mbuthia na Bw. Samson Ongarora kwa mawaidha, ushauri na uongozi wao. Mungu awabariki.

Shukran zangu maalum ninatoa kwa Dkt. Timothy Arege ambaye alinifaa kwa kunielekeza katika harakati za awali za utafiti huu. Pia alikuwa tayari kutoa ushauri wake wakati wowote na kwa kunisaidia na vitabu vya marejeleo. Mungu akubariki.

Nawashukuru wahadhiri wangu wote katika idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Nairobi, kwa mafunzo na mawaidha yao. Hawa ni pamoja na Prof. Abdulaziz, Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Kyallo Wamitila, Prof. John Habwe, Prof. Rayya Timmamy, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Kinene wa Mutiso, Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Ayub Mukhwana na Mwalimu Basilio Mungania.

Pia Shukrani zangu ziwaendee wanafunzi wenzangu ambao tulikuwa pamoja katika safari hii ya masomo. Hawa ni: Rita Magara, Rosemary Kamwanza, Rose Dama, Henry Indidi, Hezekiel Gikambi, Makhulo Evans, Otuchi Timothy, Stephen Machira na Gathara Francisco. Naomba Mola awazidishie baraka zake. Kwa Rita na Rosemary asanteni kwa ushauri wenu wenye busara.

Sitasahau kumshukuru binti yangu kipenzi, Rehema Kwamboka, ambaye kwa sababu yake ninaishi na kung'ang'ana katika maisha. Asante mwanangu kwa kuvumilia wakati mwingi uliponikosa. Mwisho na muhimu ni wazazi wangu, bwana Salim Khamis na bi. Mwanajuma Salim kwa malezi mema na kwa dua zao za mara kwa mara. Pia na ndugu zangu wote kwa kunifaa nilipowahitaji. Kuna wengine ambao walinifaa na singeweza kuwataja kwa sababu ni wengi; kwenu nyote ninatoa shukrani zangu za dhati.

# IKISIRI

Utafiti huu umeshughukilia usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* kwa kutumia nadharia ya naratolojia kwa mtazamo wa Genette (1972-1983). Utafiti huu una malengo mawili: Kwanza, kubainisha vipengele vya usimulizi. Pili, kujadili dhima ya vipengele vya usimulizi katika tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Vipengele vilivyochunguzwa ni pamoja na kipengele cha wakati, daraja na sauti za usimulizi na wahusika na uhusika. Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo: (i) Usimulizi unadhihirika katika tamthilia. (ii) Vipengele vya usimulizi hutekeleza dhima maalum katika tamthilia. Kutokana na utafiti wetu nadharia tete zetu zimethibitika. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa usimulizi upo katika tamthilia na imebainika kuwa vipengele vya usimulizi vina dhima muhimu katika kusimulia hadithi na kupitishia maudhui na dhamira katika tamthilia kama ilivyo katika riwaya na hadithi fupi.

## YALIYOMO


Ikirari ........................................................................................................................ii

Tabaruku ...................................................................................................................... iii

Shukrani ......................................................................................................................iv

Ikisiri ............................................................................................................................v

**SURA YA KWANZA ....................................................................................................1**

1.0 UTANGULIZI ...........................................................................................................1

1.1 Tatizo la Utafiti ........................................................................................................3

1.2 Madhumuni ya Utafiti ..............................................................................................4

1.3 Maswali ya Utafiti ....................................................................................................4

1.4 Nadharia Tete ...........................................................................................................4

1.5 Sababu za Kuchagua Mada .......................................................................................4

1.6 Upeo na Mipaka ........................................................................................................5

1.7 Msingi wa Kinadharia wa Utafiti ...............................................................................5

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ...................................................................................7

1.9 Mbinu za Utafiti ........................................................................................................9

**SURA YA PILI:WAKATI ...........................................................................................11**

2.0 UTANGULIZI .........................................................................................................11

2.1 Mpangilio ...............................................................................................................11

2.1.1Analepsia .............................................................................................................12

2.1.1.1 Analepsia Tawasifu ...........................................................................................13

2.1.1.2 Analepsia Wasifu .............................................................................................14

2.1.1.3 Analepsia ya Nje ..............................................................................................16

2.1.1.4 Analepsia ya Ndani ...........................................................................................18

2.1.1.5 Analepsia Mseto ...............................................................................................19

2.1.2 Prolepsia ...............................................................................................................20

2.1.2.1 Prolepsia Tawasifu ............................................................................................21

2.1.2.2 Prolepsia Wasifu ...............................................................................................22

2.1.2.3 Prolepsia ya Nje ................................................................................................23

2.1.2.4 Prolepsia ya Ndani ............................................................................................24

2.1.2.5 Prolepsia ya Mseto ............................................................................................26

2.2 Muda ........................................................................................................................27
2.2.1 Muhtasari..............................................................................................................27
2.2.2 Mtuo ......................................................................................................................28
2.2.3 Onyesho.................................................................................................................29
2.2.4 Udondoshi .............................................................................................................30
2.2.4.1 Udondoshi Bayana ..............................................................................................30
2.2.4.2 Udondoshi uso Kikomo.......................................................................................31
2.2.4.3 Udondoshi Dhahiri ..............................................................................................32
2.2.4.4 Udondoshi Batini.................................................................................................32
2.3 Idadi Marudio.............................................................................................................33
2.3.1 Usimulizi Mosi .....................................................................................................33
2.3.2 Usimulizi Rudufu .................................................................................................34
2.3.3 Usimulizi Banifu ..................................................................................................34

**SURA YA TATU:DARAJA NA SAUTI ZA USIMULIZI....................................37**
3.0 UTANGULIZI ..............................................................................................................37
3.1 Aina za Daraja zaUsimulizi ......................................................................................38
3.1.1 Daraja ya Kwanza ................................................................................................38
3.1.2 Daraja ya Pili ........................................................................................................38
3.1.3 Daraja ya Tatu ......................................................................................................39
3.2 Dhima za Hadithi Tegemezi katika Kijiba cha Moyo na Mstahiki Meya .............39
3.2.1 Dhima ya Kiutekelezaji .........................................................................................39
3.2.2 Dhima ya Kiufafanuzi ..........................................................................................40
3.2.3 Dhima ya Kimaudhui ...........................................................................................40
3.3 Metalepsia...................................................................................................................41
3.3.1 Badiliko la Usimulizi LililoWazi .........................................................................42
3.3.2 Badiliko la Usimulizi Lisilo Wazi........................................................................43
3.4 Uhusiano wa Kiwakati baina ya Usimulizi na Hadithi ..........................................44
3.4.1 Usimulizi wa Kiurejeshi.......................................................................................44
3.4.2 Usimulizi Tangulizi...............................................................................................44
3.4.3 Usimulizi Sawia ...................................................................................................45
3.5 Aina za Wasimulizi.....................................................................................................45
3.5.1 Daraja ya Simulizi ................................................................................................46
3.5.2 Uhusiano wa Msimulizi na Hadithi......................................................................48

3.5.2.1 Msimulizi Tawasifu ........................................................................ 48
3.5.2.2 Msimulizi Wasifu ........................................................................... 49
3.5.3 Utambulisho wa Msimulizi ............................................................... 50
3.5.3.1 Maelezo ya Mandhari ..................................................................... 50
3.5.3.2 Kutambulisha Wahusika .................................................................. 51
3.5.3.3 Muhtasari wa Muda ........................................................................ 52
3.6 Wasimuliwa .......................................................................................... 52
3.6.1 Kigezo cha Daraja ya Usimulizi ........................................................ 53
3.6.2 Kigezo cha Ushiriki katika hadithi .................................................... 53

**SURA YA NNE:WAHUSIKA NA UHUSIKA ........................................................ 56**
4.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 56
4.1 Mbinu za Usawiri wa Wahusika ........................................................... 56
4.1.1 Usawiri Bainishi ................................................................................ 57
4.1.2 Usawiri Timbe ................................................................................... 58
4.1.2.1 Matendo ......................................................................................... 58
4.1.2.1.1 Tendo la Utekelezaji ..................................................................... 59
4.1.2.1.2 Tendo la kukwepa ......................................................................... 62
4.1.2.1.3 Tendo la Kunuia ........................................................................... 63
4.1.2.2 Usemi .............................................................................................. 64
4.1.2.2.1 Namna Mhusika Anavyoongea ...................................................... 64
4.1.2.2.2 Mazungumzo ya Mhusika ............................................................. 67
4.1.2.2.2.1 Mhusika na wasifu wake ............................................................ 67
4.1.2.2.2.2 Mhusika na wasifu wa mhusika mwengine .................................. 68
4.1.2.3 Muonekano wa Nje ......................................................................... 69
4.1.2.3.1 Maumbile ...................................................................................... 69
4.1.2.3.2 Mavazi .......................................................................................... 70
4.1.2.4 Mazingira ....................................................................................... 71
4.1.2.5 Analojia .......................................................................................... 73
4.1.2.5.1 Majazi ........................................................................................... 73
4.1.2.5.2 Ulinganuzi wa Wahusika .............................................................. 74

**SURA YA TANO:MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO .................................76**

5.0 UTANGULIZI ..........................................................................................76

5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ............................................................76

5.3 Mapendekezo ............................................................................................79

MAREJELEO ................................................................................................80

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Fasihi* (2003), usimulizi ni uelezeaji wa matukio katika hadithi. Katika kazi yoyote ya fasihi huwa kuna kisa au hadithi fulani inayosimuliwa na msimulizi. Genette (1980), ameielezea dhana ya usimulizi kwa kurejelea mambo matatu nayo ni, simulizi, hadithi na usimuliaji. Simulizi ni kauli ya kisimulizi inayonuiwa kueleza tukio au matukio, hadithi ni mfuatano wa matukio yanayosimuliwa na usimuliaji ni tendo la kusimulia hadithi.

Usimulizi una historia ndefu sambamba na hadithi na umekuwa ukijadiliwa tangu enzi za akina Aristotle. Plato aliainisha aina mbili za usimulizi nazo ni diajesia (*diegesis*) na mimesia (*mimesis*). Katika diajesia mshairi hujitokeza waziwazi kama mzungumzaji. Kwa upande mwengine katika mimesia mshairi hajitokezi waziwazi huwafanya wasomaji au wasikilizaji wake kuamini kuwa sio yeye anayezungumza. Hivyo basi monolojia, dayalojia na usemi halisi ni mimesia, ilhali usemi wa taarifa ni diajesia. Diajesia pia inajulikana kama kueleza na mimesia kama kuonyesha.

Tamthilia hutia mkazo mkubwa sana kwenye uonyeshi (mimesia), kuwasilisha wahusika kimatendo kwa hivyo sifa ya kisimulizi haichukui nafasi kubwa sana kama ilivyo katika riwaya. Hii haina maana kuwa usimulizi hautokei. Usimulizi hutokea kupitia matini elekezi. Usimulizi unaweza pia kutokea kupitia mazungumzo ya wahusika.

Wamitila (2003) ameainisha aina zifuatazo za usimulizi:

i. Usimulizi anuwai – hii ni aina ya usimulizi ambapo pana mitazamo miwili au zaidi yaani hadithi inaweza kuwa na wasimulizi wawili au zaidi.
ii. Usimulizi ngazi – ni usimulizi ambapo kuna hadithi inayotegemezwa kwenye hadithi kuu.

iii. Usimulizi maizi – hii ni aina ya usimulizi ambapo msimulizi anaufahamu wa kila kitu kinachotokea katika hadithi.
iv. Usimulizi penyezi – hii ni aina ya usimulizi ambapo mwandishi anajitokeza mara kwa mara kutoa maoni, tathmini au mapendekezo.
v. Usimulizi sawia – hii ni aina ya usimulizi ambao huwa sawia na matukio yanayosimuliwa, yaani matendo yanatokea wakati huo huo wa usimulizi.
vi. Usimulizi tangulizi – ni usimulizi ambao unatangulia wakati wa matukio na matendo yanayosimuliwa.
vii. Usimulizi wa kiurejeshi – ni aina ya usimulizi unaosimulia matukio yaliyopita.
viii. Usimulizi wa nafsi ya kwanza – ni aina ya usimulizi ambapo msimulizi hutambulishwa na matumizi ya kiwakilishi cha nafsi ya kwanza 'mimi'.
ix. Usimuliziwa nafsi ya pili – ni aina ya usimulizi ambapo msimulizi hutambulishwa na matumizi ya kiwakilishi cha nafsi ya pili 'wewe'.
x. Usimuliziwa nafsi ya tatu – ni aina ya usimulizi ambapo msimulizi hutambulishwa na matumizi ya kiwakilishi cha nafsi ya tatu 'yeye'.

Aina hizi za usimulizi kama zilivyoainishwa na Wamitila (2003) zinaafikiana na aina za usimulizi katika naratolojia.

Genette (1980) ameainisha dhima tano za msimulizi kulingana na haja yake ya kujihusisha au kujitenga na simulizi yake. Dhima ya kwanza ni kusimulia, katika simulizi usimulizi hutekelezwa na msimulizi kama mmojawapo wa wahusika katika matini au la. Kwa mfano, katika tamthilia za Penina Muhando za *Hatia* (1962) na Nguzo *Mama* (1984) tunapata msimulizi katika matini kama mhusika.

Dhima ya pili ni kuelekeza, msimulizi anaweza kukatiza hadithi ili kuchangia katika mpangilio wa matini. Kwa mfano, kupitia maelezo ya jukwaani kwenye tamthilia. Dhima ya tatu ni kuwasiliana, msimulizi huwasiliana na msimuliwa (msomaji mtarajiwa) moja kwa moja. Dhima ya nne ni ushuhuda, msimulizi huthibitisha ukweli wa hadithi yake, uhakika kuhusu matukio na chanzo cha habari. Dhima ya tano ni itikadi, msimulizi huweza kukatiza hadithi ili kuleta maoni ya kufunza au hekima ya jumla kuhusu hadithi yake.

Utafiti huu umechunguza usimulizi katika utanzu wa tamthilia. Utanzu huu umekua kwa kasi mno na kuonyesha viwango vikubwa vya ukomavu. Tamthilia kama vile *Mashetani* (1971) na *Kijiba cha Moyo* (2009) zinadhihirisha maendeleo makubwa kwa upande wa maudhui na mbinu za kuyapitisha maudhui hayo.

Tamthilia ya Kiswahili vilevile inaonyesha uzingatiaji kaida za kirasimi za utunzi wa tamthilia kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Kinjeketile,* mbinu za Kimagharibi ambazo zinabainika katika kila tamthilia pamoja na za Kiafrika kama ilivyo katika tamthilia kama vile *Nguzo Mama* (1984).

Tasnifu hii inahusu uhakiki wa usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009). Tamthilia hizi zimeandikwa na Timothy Arege. Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) ni utungo wa kisaikolojia unaosimulia matatizo yanayoyakumba mataifa madogo huru ulimwenguni hususan ya Kiafrika. Inaangazia masuala kama vile ukoloni mamboleo, mvutano kati ya mataifa yenye uwezo mkubwa duniani, ukengeushi na mahusiano ya kifamilia.

Nayo tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009), inayotahiniwa katika shule za upili nchini Kenya, ni kazi ya kiuhalisia inayoangazia masuala kama vile uongozi mbaya, umaskini, ufisadi miongoni mwa wafanyakazi wa serikali na matumizi mabaya ya mali ya umma.

### 1.1 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu unahusu usimulizi katika tamthilia kwa kuchunguza tamthilia mbili, *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009). Kimsingi usimulizi unahusishwa na kazi za nathari kama vile riwaya na hadithi fupi. Tahakiki ambazo zimefanywa kuhusu tamthilia hazijashughulikia suala la usimulizi. Wahakiki kama vile Kahiro (2005) na Mutegi (1985), wamehakiki maudhui au fani bila kuangalia usimulizi kama kipengele kimojawapo cha fani. Hali hii ndiyo iliyotufanya kutaka kuchunguza namna usimulizi unavyodhihirika katika tamthilia.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009). Utafiti huu umenuia:

i. Kubainisha vipengele vya usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009).
ii. Kujadili dhima ya vipengele vya usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009).

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

i. Je, vipengele vya usimulizi vya wakati, daraja za usimulizi, sauti za usimulizi na wahusika na uhusika vimedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009)?
ii. Je, vipengele vya usimulizi vina dhima gani katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009)?

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Usimulizi unadhihirika katika tamthilia.
ii. Vipengele vya usimulizi hutekeleza dhima maalum katika tamthilia.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Sababu ya kwanza ya kuchagua mada hii ni kuwa suala la usimulizi katika utanzu wa tamthilia halijashughulikiwa na wahakiki. Wahakiki wengi wamehakiki maudhui au fani bila kuangalia vipengele vya usimulizi na dhima yake katika tamthilia. Kama vile Were (2012), Ndege (2013) na Okwena (2013), Hivyo basi, utafiti huu ulichochewa na hamu ya kutaka kuuziba mwanya huu katika uchunguzi wa dhana ya usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009).

Sababu ya pili ni kwamba usimulizi unahusishwa na riwaya na hadithi fupi. Utafiti huu utatoa nafasi ya kuonyesha iwapo usimulizi ni kipengele muhimu katika muundo wa tamthilia.

Aidha, tamthilia mbili zilizoteuliwa hazijafanyiwa utafiti kuhusu kipengele cha usimulizi. Kwa kuzichanganua kwa kuzingatia usimulizi, utafiti huu utajaza pengo lilioachwa na watafiti watangulizi.

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza usimulizi katika *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009) kwa kutumia nadharia ya usimulizi kwa kuzingatia mtazamo wa Genette (1972 na 1983).

Utafiti huu haukuchunguza vipengele vyote vya usimulizi. Vipengele vya usimulizi ambavyo vimechunguzwa ni wakati, daraja na sauti za usimulizi na wahusika na uhusika. Katika kipengele cha wakati utafiti huu umechunguza mpangilio, muda na idadi marudio. Katika kipengele cha daraja na sauti za usimulizi umeshughulikia usimulizi katika daraja ya kwanza (*Extradiegetic*), daraja ya pili (*Intradiegetic*) na daraja ya tatu (*Metadiegetic*), umuhimu wa hadithi tegemezi, uhusiano baina ya usimulizi na hadithi, aina za wasimulizi na aina za wasimuliwa. Katika kipengele cha wahusika na uhusika, umeangazia jinsi wahusika walivyosawiriwa. Vilevile, palipotokea haja ya kuishadidia dhana fulani tumetoa mifano kutoka simulizi nyingine.

### 1.7 Msingi wa Kinadharia wa Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya usimulizi au naratolojia. Kulingana na Bal (1997) naratolojia ni nadharia ya simulizi, matini za simulizi, picha, matukio na vitu vya kitamaduni ambavyo vinaeleza hadithi. Naratolojia ni nadharia ambayo ina historia ndefu tangu wakati wa urasimi ambapo mwanafalsafa Aristotle alipotoa mawazo yake kuhusu simulizi katika kazi yake ya *Poetics* ambamo aliendeleza mawazo ya mwalimu wake Plato ya *diegesis* na *mimesis*.

Msingi muhimu wa naratolojia ni kazi za urasimu wa Kirusi katika miaka ya 1920, haswa kazi za mtaalamu wa Kirusi Vladmir Propp aliyechunguza hurafa mia moja za Kirusi katika kitabu chake kiitwacho *Morphology of the Folktale* (Mofolojia ya hurafa). Wataalamu wengine wanaorejelewa katika ukuaji wa naratolojia ni kama vile mwanaanthropolojia muundo, Claude Levi-Strauss aliyetumia usimulizi katika kuchambua muundo wa visasili, Algirdas Julien Greimas, Claude Bremond, Roland Barthes, Tzvetan Todorov.

Wataalamu wanaohusishwa sana na naratolojia ni Mieke Bal, Seymour Chatman, Dorrit Cohn, Gerard Genette na Gerard Prince. Tasnifu hii imechukua mtazamo wa Genette (1972 na 1983). Utafiti huu umezingatia mihimili ifuatayo ya nadharia ya usimulizi: wakati, uhusika na daraja na sauti za usimulizi.

Kulingana na Rimmon-Kenan (1983), wakati katika simulizi ni uhusiano wa kiufuatano kati ya hadithi na matini. Kipengele hiki cha naratolojia kinaweza kuainishwa katika aina mbili; wakati-hadithi na wakati-matini. Wakati-hadithi ni ule wakati inaochukua hadithi husika kuanzia mwanzo hadi mwisho na wakati-matini huu ni wakati inaochukua matini fulani kusomwa. Kipengele cha wakati kinahusisha mpangilio, muda na idadi marudio.

Uhusika ni usawiri wa wahusika. Rimmon-Kenan (1983) anasema kuwa usawiri wa wahusika unaweza kufanywa kwa njia mbili, tabia ya mhusika inaweza kusawiriwa kwa kuelezewa moja kwa moja na msimulizi kwa kutumia vivumishi. Namna ya pili ni kwa kumsawiri mhusika kwa njia isiyo ya moja kwa moja, msomaji huachwa kuamua tabia ya mhusika kupitia matendo, kauli zake au kauli za wahusika wengine, muonekano wa nje, mazingira na majazi.

Athari mbalimbali za kiusomi hutokana na mabadiliko katika daraja za usimulizi. Katika ploti kuu, mwandishi anaweza kuingiza hadithi zingine fupi zikielezwa na wasimulizi wengine kutoka mwelekeo mwengine tofauti na ule wa ploti kuu. Yaani

kunaweza kuwa na hadithi ndani ya hadithi au hata hadithi mbili ambazo zinasimuliwa sambamba.

Genette (1980) ameainisha aina tatu za daraja za simulizi, daraja ya kwanza ameiita *extradiegetic* ambayo ndiyo ploti kuu. Daraja ya pili ni *intradiegetic* na Daraja ya tatu ni *metadiegetic*. Vilevile ameainisha msimulizi na msimuliwa wa daraja ya kwanza, pili, na tatu. Msimulizi na msimuliwa wa ndani (*homodiegetic*) na nje (*heterodiegetic*). Daraja na sauti za usimulizi zitaelezwa kwa kina katika sura ya tatu.

Nadharia hii husaidia kuelewa, kuchanganua na kutathmini simulizi, hii ndiyo sababu iliyopelekea kuchagua nadharia hii kuchunguza dhana ya usimulizi katika utafiti huu.

### 1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Ong'ondi (2005), ameshughulikia usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi. Ameshughulikia usimulizi wa hadithi ya *Walenisi* kwa kuchanganua vipengee vya usimulizi vya mtazamo, msimulizi wa hadithi, wakati, mpangilio wa hadithi na mbinu za unenaji. Kazi yake imetufaa sana katika kuchanganua vipengele vya usimulizi vya wakati, mpangilio na msimulizi wa hadithi. Tofauti na utafiti wa Ong'ondi ambao umeshughulikia usimulizi katika utanzu wa riwaya, utafiti huu umeshughulikia usimulizi katika utanzu wa tamthilia.

Shitemi (2011), ameshughulikia usimulizi katika Utenzi wa *Siri li Asirali* kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Amechunguza kipengele cha aina za usimulizi, mtazamo ndani na nje, wakati na vipengele vyake vya mpangilio na idadi marudio, kipengele cha mawazo na usemi. Utafiti wake umetufaa kwani utafiti huu pia umechunguza kipengele cha usimulizi cha wakati na vipengele vyake vya mpangilio na idadi marudio. Tofauti na utafiti wa Shitemi, utafiti huu umechunguza usimulizi katika tamthilia.

Arege (2012), ameshughulikia usimulizi katika utenzi wa *Rasi'l Ghuli* kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Ameshughulikia kipengele cha wakati na vipengele vyake vya mpangilio, muda na idadi marudio. Ameshughulikia pia daraja za usimulizi na wahusika. Utafiti wake umetufaa katika kuelewa vipengele vya nadharia ya naratolojia. Katika utafiti huu umeshughulikia kipengele cha usimulizi cha wakati na vipengele vyake vya mpangilio, muda na idadi marudio. Utafiti huu pia umeshughulikia daraja na sauti za usimulizi na uhusika. Tofauti na utafiti wa Arege utafiti huu umeshughulikia usimulizi katika tamthilia.

Kimani (2012) ameshughulikia, arki za simulizi bunilizi katika utenzi wa *Mikidadi na Mayasa*. Ameshughulikia sampuli za usimulizi, uhusika na mhusika, daraja za usimulizi, mpangilio wa matukio, mtazamo na usemi kwa kutumia nadharia ya naratolojia kwa mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002). Kazi ya Kimani imetufaa hasa katika kutalii vipengele vya usimulizi vya wakati, uhusika na daraja za usimulizi. Tofauti na utafiti wa Kimani utafiti huu umeshughulikia usimulizi katika tamthilia kwa kutumia nadharia ya naratolojia kwa mtazamo wa Genette (1980).

Were (2012), ameshughulikia fani katika tamthilia ya *Kilio cha Haki* (1981) na *Kijiba cha Moyo* (2009). Ameshughulikia wahusika, msuko na dayolojia na monolojia katika tamthilia hizo mbili. Kazi yake imetufaa katika uchambuzi wetu wa wahusika katika *Kijiba cha Moyo* (2009). Ingawaje utafiti huu haujachunguza aina za wahusika bali umechunguza usawiri wa wahusika kupitia usimulizi katika *Kijiba cha Moyo* (2009).

Ndege (2013), amechunguza ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege, *Chamchela* (2007), *Kijiba cha Moy*o (2009) na *Mstahiki Meya* (2009) kwa mtazamo wa umuundo. Ameshughulikia msuko na mchango wake katika tamthilia za Arege. Pia ameshughulikia mchango wa wahusika katika kuendeleza dhamira na maudhui. Vilevile ameshughulikia mchango wa matumizi ya lugha katika kudhihirisha ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege. Utafiti wake umetufaa wakati wa kuchunguza kipengele cha wahusika, ingawaje utafiti huu umejifunga na usawiri wa wahusika, wakati na daraja na sauti za usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na Mstahiki *Meya* (2009).

Okwena (2013), ameshughulikia matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu za Arege, *Chamchela* (2007), *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009). Utafiti huu umeshughulikia usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009) kwa kutumia nadharia ya naratolojia.

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009) imeshughulikiwa na wahakiki mbalimbali. Hata hivyo tahakiki nyingi ambazo zinapatikana kuhusu tamthilia hii ni miongozo ambayo imenuiwa kuwasaidia walimu na wanafunzi wa shule za upili kuielewa tamthilia hii ambayo inatahiniwa kwa hivi sasa katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne.

Baadhi ya walioandika miongozo kuhusu tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni pamoja na Mbuthia (2012), Omboga (2012), Mbuvi na Were (2012), King'ei, Kyalo na Mwangi (2012), Kaui (2012), Ryanga na Maina (2012) na Muturi (2012). Waandishi hawa wamehakiki tamthilia hii kwa kuzingatia vipengele vya maudhui, wahusika na matumizi ya lugha. Kwa hivyo katika tahakiki zao hawakushughulikia kipengee cha usimulizi wala hawakufuata utaratibu maalum wa kinadharia. Utafiti wetu umeshughulikia usimulizi katika tamthilia hiyo kwa kutumia nadharia ya naratolojia.

Utafiti huu umetoa mchango maalum na nyongeza kwa yale ambayo yamesemwa na wahakiki waliotutangulia kuhusu tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009).

**1.9 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu umekuwa wa maktabani. Mbinu zilizotumiwa ni kama vile kusoma tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009). Tumejikita katika kuchambua na kuviainisha vipengele vya usimulizi tunavyovichunguza katika tamthilia hizo kwa kuongozwa na nadharia ya naratolojia.

Vilevile tumesoma vitabu, majarida na tasnifu zinazohusu mada tuliyoichunguza. Aidha tumesoma vitabu vya naratolojia ili kupata maelezo zaidi juu ya vipengele vya usimulizi tulivyochunguza.

Wataalamu na wasomi wa fasihi wametufaa kwa ushauri juu ya mada hii kupitia maongezi nao. Pia tumetumia mtandao kupata taarifa zaidi juu ya mada. Hatimaye, tumechanganua data tuliyoikusanya na kuiwasilisha kwa njia ya maelezo.

# SURA YA PILI

## WAKATI

### 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii utafiti huu umechunguza suala la wakati kama kipengele kimojawapo cha usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009) na *Mstahiki Meya* (2009). Wakati ni kipengele muhimu katika simulizi yoyote. Ni katika wakati ambamo wahusika huishi, matukio hufanyika, na matendo ambayo ni kiini cha maudhui hutokea. Masuala yote katika simulizi huhusiana na hadithi kwa namna moja au nyingine. Ni kwa sababu hii kipengele cha wakati kina nafasi muhimu katika simulizi inayokifanya kuhitaji kutafitiwa.

Uchanganuzi wa wakati unahusika na maswali matatu nayo ni: Lini? Kwa muda gani? na mara ngapi? Katika kukishughulikia kipengele hiki cha naratolojia tunaangalia wakati-hadithi kwa kuulinganisha na wakati-matini.

Hapo awali wakati-matini ulichukuliwa kuwa ni ule wakati anaochukua msomaji kusoma matini fulani, hivyo basi ikawa vigumu kukadiria wakati kwani wasomaji mbalimbali wanakasi tofauti za usomaji. Hivyo basi, wataalamu wakapendekeza kuzingatiwa kwa nafasi tukio linachukua katika ukurasa kukadiria kigezo cha wakati. Kipengele cha wakati kinahusisha mpangilio, muda na idadi marudio.

### 2.1 Mpangilio

Kwa mujibu wa Genette (1980), mpangilio ni uhusiano kati ya mfuatano wa matukio katika hadithi na mpangilio wake katika simulizi. Mpangilio unajibu swali, lini? Tukio linaweza kuwa limetokea la kwanza, pili, au mwisho; kabla au baada ya wakati wa usimulizi. Kwa mfano, tunaweza kusema kuwa tukio A limetokea kabla ya B na C. Swali la kimsingi hapa ni kama uwasilishaji wa hadithi unaambatana na matukio

yanavyotokea kiwakati? Iwapo jibu ni ndio, basi tunapata mpangilio wa kiwakati. Iwapo jibu ni la, basi tunapata anakroni[1].

Msimulizi anaweza kusimulia matukio kadiri yalivyotokea kiwakati au anaweza kuyasimulia bila kuzingatia mpangilio wa yalivyotokea kiwakati. Kwa mfano, katika riwaya za kiupelelezi ambazo mara nyingi huanza na kuwepo kwa mauaji, upelelezi wa ni nani aliyetekeleza mauaji na sababu iliyopelekea mauaji huwasilishwa baadaye aghalabu mwishoni mwa hadithi kama ilivyo katika riwaya ya kiupelelezi *Mtambo wa Mauti*.

Usimulizi wa matukio usiofuata mpangilio Genette (1980) ameuita anakroni.

Wananaratolojia kama vile Genette (1980), Rimmon-Kenan (1983) na Jahn (2005) wanakubaliana kuwakuna aina mbili za anakroni:

i. Kisengere nyuma/analepsia.
ii. Kisengere mbele/prolepsia.

Katika kuchanganua anakroni utafiti huu utatumia dhana zilizopendekezwa na Genette za analepsia na prolepsia. Tamthilia hizi mbili zimedhihirisha aina zote mbili za anakroni.

### 2.1.1Analepsia

Analepsia ni mbinu ya usimulizi ambapo msimulizi anasimulia matukio yaliyotokea kabla ya tukio linalosimuliwa kuanza. Kwa mfano, katika *Mstahiki Meya* tunamwona Meya akilalamika kuwa mayai aliyoandaliwa ni madogo kisha anamuita Dida na kumuuliza, Dida anamweleza kuwa mwenye kuyaleta amesema kuwa kuku wanataga mayai madogo madogo. (uk. 8-9)

Katika mfano huu tunaona kuwa matukio haya hayakusimuliwa kulingana na yalivyotokea. Yalistahili kuanza kwa kuku kutaga mayai, mwenye mayai kuyaleta

[1]Istilahi iliyobuniwa na Genette (1980:84) kuelezea usimulizi wa matukio usiofuata mpangilio wa matukio kiwakati.

kwa Meya na kumwelezea Dida kwa nini ni madogo, Dida kuandaa mayai jikoni na kuyaleta mezani halafu ndio Meya kulalamika. Lakini katika simulizi, kwanza tunasimuliwa Meya kughadhabishwa na udogo wa mayai, kisha anamuita Dida ambaye anatoa sababu ya mayai kuwa madogo kama alivyoelezwa na mleta mayai hayo.

Kuna aina nyingi za analepsia. Aina hizi zinategemea anayesimulia kuhusu analepsia na sehemu ya simulizi ambayo analepsia inairejelea. Kwa misingi hii tunapata analepsia tawasifu (*homodiegetic*), analepsia wasifu (*heterodiegetic*), analepsia ya nje (*external analepsis*), analepsia ya ndani (*internal analepsis*) na analepsia mseto (*mixed analepsis*) kama anavyoeleza Genette (1980).

#### 2.1.1.1 Analepsia Tawasifu

Analepsia tawasifu[2] hutoa taarifa juu ya tukio au matukio yaliyopita ama juu ya mhusika anayesimuliwa, tukio au hadithi. Aina hii ya analepsia inadhihirika katika tamthilia zinazoshughulikiwa katika utafiti huu. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* Sele anasimulia juu ya safari yake baharini wakati akiongea na mkewe, Aisha. Anasema:

> **Sele:** Halafu kule baharini nilijimwaya. (*Ameathirika.*)
>
> Nikapiga mbizi. Nikapambana na mawimbi chini kwa chini. Nikapenya. Nikataka nitokezee huko wanakokaa papa. Nilipoibuka nilikuwa palee! Mbali huko. Kisha nikapumzika juu ya mawimbi kama gogo huku chini yangu maji yakipiga na kutoa povu. Mimi juu, papa chini. Siku hizo nilitaka niwe bingwa wa dunia. (*Kimya.*) (uk.2)

Dondoo hii ni analepsia tawasifu kwa sababu Sele anasimulia juu ya safari yake baharini na jinsi alivyoogelea. Matukio haya yalikwisha kutokea zamani kabla ya wakati wa sasa wa hadithi. Inatusaidia kuelewa tofauti ya kitabia inayojitokeza katika maisha ya Sele. Kupitia analepsia hii tunafahamu Sele alivyokuwa zamani kabla ya

[2]Aina hii ya analepsia Genette (1980) ameiita *Homodiegetic analepsis.*

kuugua. Analepsia tawasifu vilevile imejitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* ambapo Meya anasimulia juu ya vipande vya ardhi alivyojinyakulia na pia vile alivyomzawadia Bili. Anasema:

> **Meya:** Nisipokuwa nazo, nani atakuwa nazo? Mimi nimeuza vipande vyangu vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii. Nimebakiza vitatu incase. Wewe nilikugawia vinne. Unaweza kuuza kimoja au viwili kwa ajili hiyo. Vingine viweke kwa ajili yao hao watoto unaowahangaikia, hasa ile *prime plot*.
>
> (uk. 27)

Kupitia dondoo hii maudhui ya unyakuzi wa ardhi ya umma na ufisadi yamejitokeza. Tunapata kufahamu kuwa Meya alijinyakulia vipande vya ardhi vya umma na kuviuza na pia alimzawadia Bili vipande vinne vya ardhi. Matukio haya hayakusimuliwa wakati yalipokuwa yakitokea, yamekuja kusimuliwa baaye baada ya kutokea. Mazungumzo haya pia yanamsaidia msomaji kufahamu Meya ni mtu wa aina gani.

#### 2.1.1.2 Analepsia Wasifu

Analepsia wasifu[3] inatoa taarifa juu ya matukio yaliyopita ama juu ya mhusika mwingine, tukio jingine au hadithi nyingine ambayo haihusiani na mkondo wa hadithi inayosimuliwa katika kipindi cha "sasa" cha simulizi. Aina hii ya analepsia imejitokeza katika *Kijiba cha Moyo* kupitia mazungumzo ya Zainabu na Bi.Rahma ambapo hadithi inakatizwa kwa muda kidogo kwa kuingizwa masimulizi juu ya mhusika mwingine ambaye hayupo. Zainabu anamueleza Bi.Rahma juu ya hali ya Sele kama ifuatavyo:

> **Bi. Rahma:** Vipi watoto?

---

[3]Aina hii ya analepsia Genette (1980) ameiita *Heterodiegetic analepsis.*

| | |
|---|---|
| **Zainabu:** | Hawana neno ila Sele kidogo anatutia wasiwasi. |
| **Bi. Rahma:** | (*Kwa mshangao*) Wasiwasi? |
| **Zainabu:** | Si...ni kama...kama tunamwona kama anayeumwa lakini yeye anasema haumwi. |
| **Bi. Rahma:** | Wala ugonjwa haumlazi ndani? |
| **Zainabu:** | Hata kidogo! Ila mara nyingi huwa mumo humo ndani peke yake. (*Kimya*) Ni kama anayejitenga na watu... |
| **Bi. Rahma:** | Kumbe ndio maana kwangu hatii guu. |
| **Zainabu:** | Ingawa halalamiki kuumwa popote, hamu ya chakula imemwisha. Mara nyingi anakitazama tu na kama akila basi atakigusagusa mara mbili tatu na kukiacha... (uk. 13-14) |

Kupitia mazungumzo haya tunapata taswira ya hali ya Sele kupitia usemi wa Zainabu. Mathalan tunaona kuwa anajitenga na watu na hakichangamkii chakula. Hali hii inawatia kiwewe wazee hawa na kuzua mgogoro wa kimawazo unaowapelekea kujadiliana kwa kutaka kujua shida ya Sele na utatuzi wake.

Vilevile analepsia wasifu inajitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kupitia mazungumzo ya Meya na Bili. Wanasema:

| | |
|---|---|
| **Bili:** | Vipi mama? Hivi alishapata mgeni au vipi? |
| **Meya:** | Bado. Karibuni. |
| **Bili:** | (*Kwa bashasha*.) Mara ile ya mwisho tulipokuwa pamoja alionekana amechoka sana! |
| **Meya:** | Mama alisafiri ng’ambo. Madaktari wetu hawa wakubabaisha tu... (uk. 27) |

Dondoo hii inakuwa analepsia wasifu kwa sababu Meya na Bili wanajadili matukio yaliyopita kumhusu mke wa Meya. Kupitia analepsia hii tunapata kufahamu kuwa mke wa Meya ni mjamzito na amesafiri ng’ambo kwenda kujifungua. Pia inapitisha

maudhui ya usaliti miongoni mwa viongozi. Badala ya Meya kuboresha hali ya afya katika eneo lake anapeleka familia yake ng'ambo kwa matibabu. Meya hana Imani na madaktari wa kwao, haya yanadhihirika kupitia kauli yake, "Madaktari wetu hawa wakubababaisha tu." Hali ya afya Cheneo imezorota kiwango cha kuwa watu wanakufa kila siku kwa sababu ya ukosefu wa dawa hospitalini na Meya anaonekana kutojali.

### 2.1.1.3 Analepsia ya Nje

Analepsia ya nje inasimulia matukio yaliyotokea kabla ya wakati wa kuanza hadithi. Aina hii ya analepsia ya nje inajitokeza katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* pale Amri anapomsimulia Musa mchezo wake wa utotoni na tiara. Mchezo huu wa Musa ulitokea kabla ya mwanzo wa hadithi. Anasimulia ifuatavyo:

> **Amri:** Yalikufika. Nayakumbuka mimi kwa kuwa niliyabeba mimi yaliyokusumbua. Wewe ulishangilia na wenzako tiara ulipoiinua juu. Ikawa inayumbishwa na upepo na ukafurahia kushikilia uzi ulioifunga. Ukaionea tiara raha kwa kuwa huru kule juu. Uzi ulipokatika tiara ilirushwa juu zaidi kule angani. Hukufurahi. Ulikasirika. Ndipo hasa ulipolia.
>
> **Musa:** Ningelia kwa nini na si mimi niliyeikata kamba? (*Amri anacheka kwa muda*.)
>
> **Amri:** Hukulia kwa kamba kukatika. Ulilia nafsi yako
>
> ilipotambua kuwa tiara ilikuwa na uhuru kamili. Ukichunguza vizuri, si wewe uliyelia. Ni nafsi yako iliyotambua kuwa tiara haikuwa chini ya udhibiti wako. Hakuna apendaye uhuru kamili. Uhuru kamili huweza kumtoa mtu machozi. (uk.65)

Kupitia kwa maelezo ya Amri tunapata kufahamu juu ya michezo ya utotoni ya Musa ambapo tunaelezwa alicheza na tiara. Mchezo huu alicheza hata kabla ya Sele kuzaliwa na hadithi kuanza. Kupita kule kufurahi kwa Musa wakati tiara ilipokuwa inayumbishwa na upepo wakati ameshikilia uzi kunaashiria furaha yake kuyadhibiti maisha ya Sele. Ugonjwa wa Sele na kule kutaka kuwa huru ni mfano wa uzi kukatika na tiara kuwa huru. Jambo hili linawatia huzuni wazazi wake Sele. Ndiposa

tunawaona wakifuatilia maisha ya Sele, hata pale Sele mwenyewe anapowaeleza kuwa yeye si mgonjwa.

Vilevile analepsia ya nje inajitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* pale Mama anapohojiwa na daktari kuhusu chanzo cha ugonjwa wa mtoto wake. Ugonjwa ulianza kabla ya kuanza kwa hadithi kuu. Anatueleza kuwa alimpatia wali na maharagwe yalolala aliyoyapata kutoka kwa Meya, anakofanya kazi. Tunaelezwa:

| | |
|---|---|
| **Mama:** | Jana jioni baada ya chajio. Asubuhi nimeondoka kwenda kazini na niliporudi nikaona anazidi. Na leo…Afadhali jana. (*Daktari anachukua karatasi. Anamsaili huku akiandika*.) |
| **Siki:** | Jina? |
| **Mama:** | Dadavuo Kaole. |
| **Siki:** | Umri? |
| **Mama:** | Miaka mitatu. |
| **Siki:** | (*Akimtazama mama*.) Ulimlisha nini? |
| **Mama:** | Chakula. |
| **Waridi:** | (*Ameelekea kuudhika*.) Chakula gani? |
| **Mama:** | Nilichotoa kwa bwana. |
| **Siki:** | (*Akimtazama*) Kwa bwana? |
| **Mama:** | Eeh! Ninakofanya kazi. |
| **Siki:** | Unafanya kazi wapi? |
| **Mama:** | Kwa Mstahiki Meya. |
| | (*Kimya cha muda*.) |
| **Waridi:** | Chakula gani hicho hasa ulichochukua kumpa mtoto? |
| **Mama:** | Wali na maharagwe yalolala. |
| **Waridi:** | Wewe hukuyala? |
| **Mama:** | Sikuyala mie. Yalikuwa machache tu! |
| **Waridi:** | Wala hukukitokosa chakula hicho tena nyumbani? |
| **Mama:** | (*Akimtazama*.) Moto utatoka wapi |

> mwanangu? Makaa siku hizi yamepanda bei tangu sheria ya misitu ishike kasi. Nayo bei ya mafuta taa ndiyo hiyo inapanda kila uchao. (uk.4-5)

Kupitia mahojiano haya tunapata kufahamu chanzo cha ugonjwa wa Dadavuo Kaole. Pia maudhui ya umasikini yanajitokeza kupitia kitendo cha Mama cha kumpa mwanawe maharagwe na wali uliolala. Hakuweza kukipasha chakula moto kutokana na ukosefu wa makaa na mafuta ya taa. Mama ni mfanyakazi wa Meya lakini Meya hajali maslahi ya wafanyakazi wake.

### 2.1.1.4 Analepsia ya Ndani

Analepsia ya ndani inasimulia matukio yaliyotokea baada ya kuanza kwa hadithi lakini yanayosimuliwa baadaye katika hadithi wala sio wakati ule yalipotokea. Analepsia ya ndani imejitokeza katika sehemu IV, onyesho II katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ambapo mtiririko wa hadithi unakatizwa na tunasimuliwa matukio yaliyotokea hapo nyuma, matukio yenyewe hayakusimuliwa wakati ule yalipokuwa yanatukia yamekuja kusimuliwa baadaye kupitia Sele. Sele alimsimulia Zainabu juu ya waganga waliokuja nyumbani kwake kumtibu. Kupitia analepsia hii ndipo tunapata ufahamu wa kuja kwa madaktari na mganga kumtibu Sele.

> **Sele:** (*Baada ya kimya*) Basi hiyo jana wamekuja wote watatu. Mimi nimelala chumbani. Yule daktari mrefu amefika akiongoza na yule mfupi nyuma yake anamfuata. Na hatua kadhaa nyuma yao yule mganga. Yeye anatembea kama asiye na hakika na hatua zake. Mwanzo nilidhani yeye mgonjwa. Nilipokuwa namtazama kwa makini kutoka mle kitandani, mara nawaona wale madaktari wawili wamesimama wanatazamana. Si mbali na mimi. Nikaona ni kama wanajibizana kwa furaha kuu na kukumbatiana. Halafu ghafla naona kama wanazozana. Yule mrefu anaongea kwa sauti ya kulalamika na kutisha. Yule mfupi anamtazama na kumjibu mara moja moja kwa sauti ya chini. Sikupata kusikia alichosema. Lakini niliona kitu kimoja kilichonishangaza. (*Kimya*)... (uk. 79-81)

Dondoo hii inatoa taarifa ya madaktari na mganga wanaomng'ang'ania mgonjwa kutaka kumtibu kila mmoja akiwa na dhamira yake. Madaktari na mganga hapa wametumika kisitiari. Madaktari wanawakilisha mataifa ya kigeni na mganga anawakilisha mataifa ya Kiafrika na mgonjwa anawakilisha nchi ya Kiafrika inayozozaniwa.

Katika *Mstahiki Meya* analepsia ya ndani imejitokeza pale ambapo daktari Siki anamuelezea Meya kilichomtokea siku iliyopita. Anasema, "Kweli. Ni jana tu kitoto kidogo kimenifia mkononi mwangu kwa njaa na ugonjwa..." (uk.12). Tukio hili limetokea wakati uliopita. Hii inadhihirika kupitia matumizi ya neno "jana". Usemi huu unadhihirisha maudhui ya kifo kutokana na umaskini na maradhi. Hii ni hali ya kutamausha.

### 2.1.1.5 Analepsia Mseto

Analepsia mseto inasimulia matukio yaliyotokea kabla ya simulizi ya mwanzo na kuendelea hadi mwanzo wa simulizi au hata kuvuka mwanzo wa simulizi hiyo (Rimmon-Kenan 1983). Katika *Kijiba cha Moyo* kuna analepsia mseto pale ambapo Sele anasimulia juu ya maisha yake ya utotoni. Analepsia hii inaturudisha nyuma hadi siku ile Sele alipozaliwa, siku zake za utotoni, alipokuwa shuleni na hatimaye kuturudisha tena katika wakati wa sasa wa hadithi.

**Sele:** Sikiliza bibi. Kuchekwa kwangu kulianza mara baada ya kuwasili kutoka tumboni. Na hata siku zile pua yangu ikifanya sigara mbilimbili bado nilichekwa.

**Zainabu:** Michezo yenu shuleni ndiyo bado inakusumbua akili.

**Sele:** Si michezo ya shuleni. Hata nyumbani pia.

Mlinicheka kwa mwendo wangu wa matagamataga. Mlinicheka kwa midomo yangu mikubwa. Nilichekwa kwa weusi uliokoza na kukolea. (*Kimya*.) Siku zile machozi yalinitoka kabla nianze kulia. Sasa ninalia bila machozi kutoka. Hulia ndani kwa ndani yasionekane. Na yanapotoka watu

> hudhani ni machozi ya furaha. Nami papo hapo huyafunika kwa kicheko kizito. Na katika kicheko hiki mna kitone kinachoniandama... (uk.43)

Analepsia hii inatoa taswira kamili ya maisha ya Sele, hivyo basi kumwezesha msomaji kuelewa chanzo cha shida zake.

### 2.1.2 Prolepsia

Prolepsia ni mbinu ya usimulizi ambapo msimulizi anasimulia matukio yatakayotokea baada ya muda wa "sasa" wa hadithi. Prolepsia ni tofauti na taharuki. Taharuki humuacha msomaji au mtazamaji na hamu ya kutaka kujua ni nini kitatokea baadaye ilhali prolepsia inasimulia matukio yatakayotokea baadaye kabla ya muda wake kufika.

Wamitila (2008) akimnukuu Toolan (1990) anasema, hii ni mbinu ambayo kimsingi inachujua taharuki ya hadithi inayosimuliwa kwa kuwa inasimulia matukio kabla ya ulazima wake wa kiwakati. Anaendelea kusema kuwa prolepsia inatoa mkazo kutoka kwenye taharuki ya nini hadi kwenye taharuki ya vipi, yaani msomaji hajiulizi ni nini kitakachotokea (kwa sababu anakijua) bali ni vipi kitakavyotokea.

Baadhi ya wahakiki wanaamini kuwa prolespia hutumika zaidi katika kazi zilizosimuliwa katika nafsi ya kwanza kwa kuwa inakubalika zaidi kwa msimulizi wa aina hiyo kuchupa hadi matukio ya mbeleni kuliko ilivyo katika kazi zilizosimuliwa katika nafsi ya pili au tatu (Wamitila 2008).

Prolepsia kama zilivyo analepsia zinaweza kuainishwa kama prolepsia tawasifu na prolepsia wasifu. Vilevile kunazo prolepsia za nje, Prolepsia za ndani na prolepsia mseto (Genette 1980). Prolepsia hazijitokezi kwa wingi katika simulizi kama zinavyojitokeza analepsia. Aghalabu hutumika kuzua taharuki (Bal 1997).

#### 2.1.2.1 Prolepsia Tawasifu

Prolepsia tawasifu ni aina ya prolepsia ambayo hutoa taarifa juu ya matukio yanayokuja ama juu ya mhusika, tukio au hadithi inayosimuliwa katika wakati wa sasa wa hadithi. Aina hii ya prolepsia Genette (1980) ameiita *Homodiegetic prolepsis*.

Prolepsia tawasifu imedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* pale ambapo Bi. Rahma anazungumza na Aisha na kumuonya juu ya athari za kuwapuuza wazee wake. Pia inajitokeza pale anapomuasa Sele juu ya madhara ya kufanyiwa upasuaji wa uso. Anasema:

**Bi. Rahma:** Dogo ilhali linakufanya utupuuze sisi?Usipochunga utakuja tumwa kwangu nikutie skuli. Haya! (uk.19)

.............................................................................................

**Bi. Rahma:** Utakuja chekwa hatimaye. Mimi nakwambia! (uk.43)

Dondoo ya kwanza linatupatia taswira ya utamaduni wa wahusika. Ambapo mke muolewa anapokosa nidhamu hutumwa kwa wazee wake akafunzwe. Dondoo ya pili, Bi.Rahma anaelezea kile kitakachomfanyikia Sele iwapo atafanyiwa upasuaji wa uso. Kupitia dondoo zote hizi mbili tunapata kujua matukio kabla ya muda wake wa kutokea haujafika.

Vilevile, prolepsia tawasifu imejitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* pale ambapo Bili ananuia kumpeleka mkewe ng'ambo kujifungua wakati wake wa kujifungua ukiwadia. Anasema, "Sikujua. Hata mimi sasa naona nitamtuma mke wangu huko huko wakati wake ukitimia..." (uk.27).

Nukuu hii ni prolepsia tawasifu kwa sababu, wakati wa mke wa Bili wa kujifungua haujafika na Bili hajamtuma ng'ambo kujifungua. Lakini Bili anaelezea kwamba atamtuma huko wakati wake wa kujifungua ukiwadia.

### 2.1.2.2 Prolepsia Wasifu

Prolepsia wasifu hutoa taarifa juu ya matukio yanayokuja ama juu ya mhusika mwingine, tukio jingine au hadithi nyingine mbali na mhusika, tukio au hadithi inayosimuliwa katika wakati wa sasa wa hadithi. Aina hii ya pili ya prolepsia, Genette (1980) ameiita *Heterodiegetic prolepsis*.

Aina hii ya prolepsia imedhihirika katika tamthilia zinazochunguzwa katika utafiti huu. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* prolepsia wasifu imejitokeza pale ambapo Meya na Bili wanazungumzia juu ya mwanakandarasi kwenda kortini. Bili anamshauri Meya amwite mwanakandarasi na amwambie aende kortini. Anasema,

> **Bili:** Wewe mwite umwambie ende kortini. Bila shaka korti itaamuru alipwe hela thamani ya pato ambalo angalipata kipindi chote cha mkataba…Hakimu ataamuru alipwe fidia. Tena sio wewe wa kulipa. Baraza litalipa maana ulichukua hatua kwa niaba ya Baraza. Kumbuka mtumwa hauawi. Muhimu ni kukubaliana naye kuhusu fungu atakalokupa kutokana na pato lake. Ukitaka hata unaweza kumtuma wakili wa Baraza waiendeshe kesi naye..." (uk.29).

Kupitia mfano huu tunaona kuwa Meya na Bili wanapanga namna mwanakandarasi ataenda kortini kushitaki na namna korti itaamua baraza kumlipa fidia mwanakandarasi. Matukio haya yote yamesimuliwa kabla ya muda wake wa kutokea.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, Zainabu anazungumzia chungu chake kuungua jikoni. Anasema, "Naja chungu changu ki<u>ta</u>ungua." Hapa kinachosimuliwa ni chungu na tendo la kuungua halijatokea katika wakati wa usimulizi. Hili linawakilishwa na mofu 'ta' ya njeo au wakati ujao.

**2.1.2.3 Prolepsia ya Nje**

Prolepsia ya nje inasimulia tukio au matukio ambayo yatatokea katika kipindi cha baada ya hadithi na haihitilafiani na simulizi ya kwanza. Proplepsia ya nje huanza na kuisha nje ya mawanda ya msuko mkuu. Msomaji ataisoma hadithi hiyo hadi mwisho bila kushuhudia kisa au tukio linalotangulizwa au kuelekezwa kwa kuwa liko nje ya mipaka hiyo ya hadithi (Wamitila 2008). Prolepsia ya nje inaweza kuwa tawasifu au wasifu.

Aina hii inajitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* pale ambapo Meya anajizungumzia juu ya kumfurusha mwanakandarasi na mipango ya mapokezi ya wageni watarajiwa. Anasema:

> Meya: ...Huyu nitamfurusha. Hatamu mpya na mipango mipya. Hata akashitaki ni bure...Nitawapa mapokezi ya kupigiwa mfano. Hoteli ya kifahari. Vyakula kutoka kila utamaduni duniani...Mvinyo nitauagizia kutoka Urusi na divai kutoka Ufaransa. Wale na kunywa wajue kuwa Cheneo si mji hivi hivi. Wauone ukarimu wetu na maana ya udugu wetu... (uk.25)

Kupitia dondoo hii tunamuona Meya akipanga mipango ya kumfurusha mwanakandarasi na mikakati ya mapokezi ya mameya kutoka nchi za nje. Yote haya hayakutokea katika hadithi, pengine yalitokea mbeleni zaidi baada ya simulizi kuisha.

Aina hii ya prolepsia ya nje pia imedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* pale ambapo kutumwa kwa Aisha kwa Bi. Rahma kutiwa skuli ambako Bi Rahma alikutanguliza katika ukurasa wa 19 hakukutokea katika hadithi.

Vilevile, prolepsia ya nje inajitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* pale ambapo Diwani III. Anasema:

> **Diwani III:** Leo itakuwa jana na jana kuwa juzi, juzi itasahaulika lakini uongozi hautasahaulika ama kwa mabaya au mazuri yake. Vizazi vitakumbuka kwa alama ulizoacha nyuma. Hawa wanaotaka uwasikilize ni mzizi wa vizazi vya kesho... (uk.55).

Diwani III anaelezea juu ya vizazi vijavyo baada ya uongozi wao. Hii ni prolepsia ya nje kwa sababu inazungumzia matukio yatakayotokea mbeleni. Hivi kwamba leo inayozungumziwa bado haijawa jana na wala vizazivya kesho havijafika.

#### 2.1.2.4 Prolepsia ya Ndani

Prolepsia ya ndani inasimulia tukio au matukio ambayo yatatokea katika kipindi kabla ya mwisho wa simulizi ya kwanza, yaani huwa katika mawanda ya hadithi inayosimuliwa bali si nje yake. Aghalabu prolepsia ya ndani inaweza kuwa tawasifu au wasifu.

Wageni wanaotarajiwa kuzuru mji wa Cheneo katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* pia ni mfano wa prolepsia ya ndani ambapo kuja kwao kumezungumziwa na wahusika mbalimbali hata kabla ya kufika kwao kama vile Diwani I (uk.23), Siki (uk.39), Diwani I (uk.50) na Meya (uk.67 na 73). Ingawaje wageni waliwasili kabla ya kuisha kwa hadithi lakini kwa sababu ya mgomo wa wafanyakazi wa kiwanda cha ndege, ndege yao ilielekezwa mji jirani wa Shuara (uk.75- 77).

Vilevile, prolepsia ya ndani imejitokeza katika tamthila ya *Mstahiki Meya* pale ambapo Waridi anazungumzia mgomo na maandamano ya wafanyakazi yalikuwa yakipangwa. Waridi anasema:

Waridi: Yangekuwa hayo tu labda ningeendelea kuhudumu lakini tangu wiki iliyopita nahisi kuna jambo ambalo haliendi sawa. Mwanzo sikujua ni nini hasa lakini jana nimepata habari kuwa huenda pakawepo migomo na maandamano siku yoyote. (uk.36)

Migomo na maandamano aliyoyazungumzia Waridi hatimaye yalifanyika baadaye kabla ya kuisha kwa hadithi. Tunapata ithibati kuwa mgomo ulitokea kupitia usemi wa Diwani III katika ukurasa 53. Anasema: "Wafanyakazi wamegoma kwa kutaka nyongeza ya mishahara ambayo hawakupewa..."

Vilevile, hili linadhihirika kupitia usemi wa Meya kuwaambia wawakilishi wa wafanyakazi alipofanya mkutano nao. Anasema:

**Meya:** Tatu, unafahamu fika kuwa hili haliwezekani. Baraza lina kanuni zake ambazo lazima ziheshimiwe. Ni mpaka kanuni hizo zifanyiwe mabadiliko. Hata kama ingekuwa kwamba hilo linawezekana hatuwezi kushiriki kikao na watu waliogoma. Tunaweza kuzungumza na watu walio kazini, si watu waliogoma. (uk.71-72).

Pia wafanyakazi katika uwanja wa ndege nao pia waligoma hatimaye. Dida anasema, "Habari zinasema wamegoma. Kuwaunga wenzao waliogoma mkono." (uk.76)

Prolepsia ya ndani imetumika kuelezea juu ya hatua za kufanya upasuaji utakavyofanyika katika *Kijiba cha Moyo*:

**Sele :** (*Akiunyosha mkononi kwa daktari*) hiyo dawa

haitanitia unyonge nishindwe kubanduka humu kitandani?

**Daktari:** Hata kidogo. Muda wote nikikushughulikia utakuwa macho. Hutahisi maumivu. Utakuwa macho. (uk.53)

Upasuaji wenyewe haujafanyika lakini kupitia usemi wa daktari tunaelezewa namna upasuaji utakavyofanyika.

#### 2.1.2.5 Prolepsia ya Mseto

Prolepsia ya mseto ni mchanganyiko wa prolepsia ya ndani na prolepsia ya nje hivi kwamba inaweza kusimulia tukio au matukio ambayo yatatokea kabla au hata baada ya simulizi ya kwanza. Vilevile inaweza kuwa tawasifu au wasifu.

Hivyo basi mpango wa Meya, Bili, Diwani I na Diwani II wa kuitorosha fimbo ya Meya na kuiuza ngambo katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* inakuwa ni prolepsia mseto. Bili anasimulia jinsi ya kuitoa fimbo ya Meya na namna ya kusingizia rabsha za wafanyakazi na kupotea kwa fimbo hiyo. Anasema:

**Bili:** Jambo dogo sana hilo. Bwana usalama tunaye hapa. Nani atathubutu kumkagua akitoka na mzigo wake? Baada ya wiki tena yeye huyo aje atangaze hadharani kwamba kufuatia rabsha zilizotokea Fimbo ya Meya imeibiwa na kuwa uchunguzi umeanzishwa mara moja. Wakati huo fimbo itakuwa tayari imeuzwa ngambo. Wakati huo huo anzisha mazungumzo na wafanyakazi na kuwafanya waonekane kuwa wao ndio wasiotaka suluhu. Atakuja kujua nani ila aambiwe na sisi? Kitu kidogo hiki. Mnaonaje? (uk.62)

Kupitia dondoo hii tunapata fununu juu ya mpango wa Meya, Bili, Diwani I na Diwani II wa kuitorosha fimbo ya Meya na kuiuza ng’ambo. Prolepsia hii imetumika kupitishia maudhui ya ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka miongoni mwa

watumishi wa umma. Aidha, inaonyesha tabia za wahusika hawa. Tukio hili la kutorosha fimbo halishuhudiwi katika hadithi.

## 2.2 Muda

Muda[4] huurejelea uhusiano wa kiwakati katika hadithi. Hapa tunajiuliza: tukio limechukua kipindi kirefu au kifupi? Kulingana na Genette (1980), ni vigumu kukadiria wakati matini hasa katika kuuhusisha na muda kuliko ilivyo katika kuulinganishana mpangilio na idadi marudio. Ni rahisi kusema kuwa tukio A limetokea kabla ya B au tukio C limesimuliwa mara mbili katika matini lakini ni vigumu kukadiria muda wa matini na muda wa hadithi. Hii ni kwa sababu hakuna njia ya kupima muda matini.

Kipimo kilichokuwa kikitumika kupima muda matini ni ule wakati anaochukua msomaji kusoma matini, na huu hutofautiana kutoka msomaji mmoja hadi mwingine. Rimmon-Kenan (1983), amependekeza dhana ya muda iangaliwe kupitia uhusiano uliopo baina ya wakati-hadithi (unaopimwa katika dakika, saa, siku, miezi au miaka) na urefu wa matini (unaopimwa katika mistari na kurasa). Uhusiano huu kati ya wakati-matini na wakati-hadithi huathiri kasi ya usimulizi.

Katika matini msimulizi anaweza kuharakisha au kupunguza kasi ya usimulizi wa matukio. Kwa mfano, maisha ya mhusika yanaweza kuelezewa kwa sentensi moja au matukio ya siku moja yanaweza kusimuliwa katika kurasa mia moja. Kulingana na Genette (1980) anasema, muda unaweza kudhihirishwa kwa namna nne; muhtasari, mtuo, onyesho na udondoshi.

### 2.2.1 Muhtasari

Katika muhtasari wakati-matini huwa mfupi kuliko wakati-hadithi. Muda wa usimulizi wa matukio huharakishwa, baadhi za nyakati za matukio hufupishwa katika

[4]Muda pia hujulikana kama wakaa. ( Wamitila 2008)

simulizi. Rimon-Kenan (1983) anatueleza kuwa kasi ya hadithi huharakishwa katika muhtasari; hili hutokana na ufupishaji wa muda fulani wa hadithi kwa kauli chache tu.

Hali hii tunaiona katika tamthilia ya *Kijiba cha moyo*. Bi. Rahma anasema:

> **Bi. Rahma:** Ulezi ni kazi. Hakuna mchezo! Lazima kujituma tangu vikiwa tumboni, vije duniani huku vyalia kama kukukashifu wewe kwa kuvileta duniani. Halafu vitambae, viketi huku udenda unavitoka na kisha vyende kwa kudema kwa viguu vyao dhaifu. Kisha viketi segemnege. Na tena ushuhudie mwenyewe vikiwa vibarubaru hadi vyenyewe hivyo uvione vijitu vizima vinafuata njia yao vipendavyo... (uk.83).

Bi. Rahma anazungumzia ulezi mzima kwa maneno machache. Anaelezea hatua za maisha ya binadamu. Kuanzia akiwa tumboni (kwa kawaida huchukua miezi tisa), aketi (kati ya miezi minne na mitano), atambae (kati ya miezi sita na minane), asimame dede (kati ya miezi tisa na mwaka mmoja), atembee kwa kudema (kati ya mwaka mmoja –mwaka mmoja na miezi miwili), awe barubaru (miaka kumi- kumi na saba) na hatimaye awe mtu mzima (miaka kumi na nane na zaidi). Hatua hizi zote zimefupishwa na kusimuliwa kwa maneno machache.

### 2.2.2 Mtuo

Mtuo ni maelezo marefu ambamo ndani yake hakuna tendo lolote linalotendeka, kwa mfano maelezo ya mandhari, fikira za mhusika na kadhalika. Katika mtuo wakati matini unaelekea kuwa mrefu kuliko ule wa hadithi. Wakati hadithi huwa nunge lakini wakati matini huwa unaendelea. Hii ndiyo kasi ya chini. Kwa mfano katika *Mstahiki Meya* wakati hadithi umekatizwa katika sehemu ya I, onyesho la II ili kuelezea taswira ya nyumbani kwa Meya.

> Siku ya pili asubuhi. Nyumbani kwa Meya. Meya ameketi mezani. Mbele yake kuna mayai kadhaa katika sahani na kikombe cha chai. Pembeni kuna makochi ya kupendeza.

Sakafuni kuna zulia lenye ruwaza za kupendeza. Vilevile kuna vyakula vya aina mbalimbali mezani. (uk.8).

Maelezo haya yanadhihirisha ukinzani uliopo baina ya maisha ya Meya na ya Wanacheneo. Kupitia maelezo haya tunaiona hali ya utajiri inayomzingira Meya. Hali hii inakinzana na hali ya umaskini inayosimuliwa katika hadithi. Umaskini unajitokeza kupitia mamake Dadavuo Kaole ambaye amempa mwanawe wali na maharagwe yaliyolala aliyoyatoa kwa Meya. Anashindwa hata kukitokosa chakula hicho kwa kukosa makaa na mafuta ya taa kwa sababu ya umaskini.

### 2.2.3 Onyesho

Katika onyesho wakati-hadithi na wakati-matini huwa sawa. Katika onyesho matendo na mazungumzo hutokea sambamba. Mfano mzuri wa onyesho ni dayolojia. Mazungumzo ni njia mojawapo ya kulidhihirisha onyesho. Kimsingi drama hutegemea uwasilishaji wa maneno ya wahusika kwa njia ya kimatendo. Hivyo basi onyesho ndicho kipashio muhimu katika muundo wa kidrama. Onyesho linapaswa kuwaendeleza wahusika, dhamira, maudhui na msuko. Tamthilia zote mbili zimesheheni dayolojia baina ya wahusika. Kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, onyesho linadhihirika ifuatavyo:

**Meya:** (*Kwa ukali*) Uongo!

**Siki:** Kweli. Jana tu kitoto kidogo kimenifia mkononi mwangu kwa njaa na ugonjwa.

**Meya:** Huyo mmoja tu? (*Kimya*) Unadhani wangapi wananiunga mkono? (*Akigonga meza*) Cheneo ina watu wangapi?

**Siki:** Bwana Meya, mimi ninakwambia kama ndugu yako. Sisemi kwa sababu ya siasa. La! Ukweli ni kwamba watu wetu wana tatizo. Watu wetu wana njaa. Wana kiu ambayo haikuzimwa. Ni hatari kuwaongoza watu wenye kukosa haya mawili. Huenda isichukue muda mrefu...

**Meya:** (*Ana wasiwasi*) Umesema nini Siki? Huheshimu uongozi wangu? Huoni niliyoyafanya hapa Cheneo?

**Siki:** Iwapo umefanya, yapo mengi ambayo hayakunyoka. Yanakungoja wewe na wenzako kuyanyoosha. (*Kimya*) Watu hii leo wanakufa kwa kula mizizi na matunda mwitu! Watu wako ndugu Sosi. Watu unaowaongoza wewe. (uk.12)

Kupitia mazungumzo hayo ya daktari Siki na Meya, maudhui ya kifo, njaa, ugonjwa, umaskini na masuala ya uongozi yamejitokeza. Kupitia mazungumzo haya pia sifa za wahusika wenyewe zimebainika. Mathalan, daktari Siki amedhihirika kama mshauri na mtu mwenye kujali maslahi ya watu wengine ilhali Meya amejidhihirisha kama kiongozi asiyejali shida za watu anaowaongoza.

### 2.2.4 Udondoshi

Hii ndiyo kasi ya juu zaidi kwa mujibu wa Genette (1980), Wakati-matini huwa nunge ilhali wakati-hadithi unaendelea. Baadhi ya matukio hudondoshwa na kutosimuliwa katika matini. Kuna aina mbili za udondoshi: Udondoshi bayana (*definite ellipsis*) na Udondoshi uso kikomo (*indefinite ellipsis*). Kwa mujibu wa Genette (1980) udondoshi unaweza kuwa dhahiri (*explicit*) au batini (*implicit*).

#### 2.2.4.1 Udondoshi Bayana

Udondoshi bayana unaonyeshwa kwa kusimulia waziwazi muda uliorukwa. Wakati wa onyesho unaweza kudokezwa waziwazi katika maelekezo ya jukwaani kwa maneno au vishazi fulani (alasiri, siku hiyo usiku, siku ya pili, baada ya miezi mitatu n.k). Katika *Mstahiki Meya* matukio baina ya Sehemu I na Sehemu II yameharakishwa na wakati umefupishwa katika simulizi. Kuna matukio ambayo yalitokea ambayo hayakusimuliwa.

> Asubuhi. Umepita mwezi mmoja. Meya amefika ofisini kupanga mikakati ya mapokezi ya mameya kutoka nchi za nje. Anayapitiapitia mafaili yaliyo mezani mwake. (uk.25).

Huu ni udondoshi bayana. Katika onyesho lililotangulia Sehemu ya I onyesho la III matukio yalitokea siku moja na matukio katika onyesho la II. Baina ya Onyesho II na la I katika sehemu I imepita siku moja tu. Onyesho II linaanza kwa (*siku ya pili asubuhi*...) Onyesho la III linaanza na (*Siku hiyo hiyo alasiri*...) Hii inaonyesha kuwa matukio katika onyesho I na II yametokea siku moja ilhali onyesho linalofuata, onyesho I sehemu ya II tunaelezwa kuwa umepita mwezi. Hivyo basi matukio ya mwezi mzima hayakusimuliwa.

Udondoshi bayana vilevile umedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, kwa mfano tunaelezwa: "Siku inayofuata asubuhi. Hospitalini..." Hii inaonyesha kuwa kuna matukio ya usiku mmoja baina ya onyesho I na II sehemu ya III ambayo yamedondoshwa.

**2.2.4.2 Udondoshi uso Kikomo**

Udondoshi uso kikomo hauonyeshi muda halisi. Hutumia maneno kama vile, miaka mingi baadaye, milele, muda kidogo, na kadhalika. Udondoshi huu umedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Aisha:** | (*Baada ya kimya*.) Kuzivalia njuga hakutoshi? |
| **Sele:** | Hakutoshi! Zinataka muda kabla ya kujitosa mzima mzima ukumbini kuzicheza... (uk.12) |

Katika dondoo hii, neno muda limetumika kuwakilisha wakati ambao sio bayana. Hatujaelezewa kama ni saa, siku, miezi au miaka.

Udondoshi uso kikomo vilevile umedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. Katika Sehemu ya II Onyesho la I kupitia kwa matini elekezi tunafahamishwa kuwa "Siku kadhaa zimepita. Ni adhuhuri..." (uk.31). Siku kadhaa inaweza kumaanisha siku mbili, tatu, kumi au hata zaidi zimepita. Kiwango halisi cha muda hakijaelezwa. Lakini tunafahamu kuwa kuna matukio ya siku nyingi ambayo hayakusimuliwa.

#### 2.2.4.3 Udondoshi Dhahiri

Udondoshi dhahiri unaweza kuwa ama bayana au uso kikomo. Katika aina hii ya udondoshi, matini inataja waziwazi kuwa muda wa hadithi umepita. Kwa mfano, katika *Kijiba cha Moyo* kupitia matini elekezi muda unatambulishwa kama ifuatavyo, "Siku inayofuata asubuhi. Hospitalini." (uk.59). Hii ina maana kuwa kuna matukio ambayo yametokea usiku wa kuamkia siku hiyo ya pili asubuhi ambayo yamedondoshwa.

Aidha, katika *Kijiba cha Moyo* udondoshi dhahiri unajitokeza kupitia matini elekezi. Tunafahamishwa, "Baada ya siku chache kupita..." (uk.76). Hii ina maana kuwa kuna matukio ya siku kadhaa (si wazi kama ni siku mbili au tatu) ambayo yametokea lakini yamedondoshwa. Mfano mwengine unajitokeza katika *Mstahiki Meya* kupitia matini elekezi ambapo baina ya matukio katika sehemu I na II umepita mwezi mzima. Msimulizi anasema:

> Asubuhi. Umepita mwezi mmoja. Meya amefika ofisini kupanga mikakati ya mapokezi ya mameyakutoka nchi za nje. Anayapitia mafaili yaliyo mezani. (uk.25).

Hadithi imeharakishwa hivi kwamba baada ya mazungumzo ya Meya na daktari Siki nyumbani kwa Meya (Onyesho I uk 8-15) na mkutano wa Meya na wanakamati wa Kamati ya Meya ofisini mwa Meya (onyesho II uk 16-24) ambayo yalichukua siku moja, matukio ya mwezi mzima baadaye yalidondoshwa.

#### 2.2.4.4 Udondoshi Batini

Udondoshi batini hausemi chochote juu ya muda ambao umepita. Msomaji anatakiwa abaini mwenyewe kuwa muda fulani umepita baina ya matukio lakini anaweza kufanya hivyo baada ya kugundua kuwa kuna mwanya wa kiwakati katika mfululizo wa hadithi. Udondoshi wa aina hii unajitokeza katika *Kijiba cha Moyo* pale ambapo Bi. Rahma anamtuma Aisha kwenda kumwita Jamila (uk.85) na baada ya hapo hatuelezwi chochote hadi pale tunawaona Bi. Rahma na Zainabu wakimngoja Jamila kutoka chumbani kwa Sele (uk.88-92). Bila shaka muda umepita tangu Aisha aende

kumuita Jamila, Jamila kuja nyumbani kwa Sele hadi pale anatoka chumbani na kuongea na akina Bi. Rahma na Zainabu juu ya ugonjwa wa Sele ingawaje muda wote huu haukusimuliwa.

Vilevile, katika *Kijiba cha Moyo* sehemu ya VI onyesho la I kupitia matini elekezi tunafahamishwa kuwa, “Jioni moja. Nyumbani kwa Sele...” Wakati hapa si dhahiri lakini tunafahamu kuwa kuna muda fulani ambao umepita ingawaje si dhahiri. (uk.83).

### 2.3 Idadi Marudio

Dhana ya idadi marudio [5] inarejelea tukio limetokea mara ngapi katika hadithi na limesimuliwa mara ngapi katika matini. Wamitila (2002) ameiita dhana hii umara. Wamitila anaeleza kwamba umara huhusisha urudiaji kwa kiasi fulani. Genette (1980) ameainisha aina tatu za idadi marudio; usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu.

#### 2.3.1 Usimulizi Mosi

Katika aina hii ya usimulizi tukio hutokea mara moja na kusimuliwa mara moja vilevile katika matini. Hii ndiyo aina maarufu ya usimulizi katika matini za simulizi ambayo pia inapatikana katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* na tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. Maonyesho mengi yametumia usimulizi huu. Kwa mfano katika *Kijiba cha Moyo* kucheza muziki kwa Sele na Aisha (uk.7-10), Zainabu kusafisha vyombo karoni (uk.23) na kadhalika. Yote haya yalitokea mara moja na kusimuliwa mara moja tu.

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* imesheheni mifano mingi ya aina hii ya usimulizi mathalan: Matukio baina ya daktari Siki, Waridi na mamake Dadavuo Kaole yametokea mara moja kule hospitalini na yamesimuliwa mara moja vilevile (uk.1-7). Vilevile tukio la Meya kukabwa na yai na kuchomwa na chai moto lilitokea mara

[5]Dhana hii pia inajulikana kama umara. (Wamitila 2008).

moja nyumbani kwa Meya na limesimuliwa mara moja tu (uk.8). Mkutano wa dharura baina ya Meya na wanakamati wote wa Kamati ya Meya (uk.16-24), tukio la Waridi la kuacha kazi (uk.36), mazungumzo baina ya daktari Siki na Tatu (uk.37-40), mkutano wa Meya na mhubiri (uk.41-44), mkutano wa daktari Siki na Diwani III (uk.45-51), mkutano wa Meya na wawakilishi wa wafanyakazi (uk.66-72) na kadhalika. Matukio haya yote yametokea mara moja moja na kusimuliwa mara moja moja tu katika hadithi.

### 2.3.2 Usimulizi Rudufu

Katika aina hii ya usimulizi tukio lililotokea mara moja linasimuliwa mara kadhaa katika matini. Kwa mfano, kuachishwa kazi kwa Sele kulitokea mara moja lakini katika hadithi nzima kumesimuliwa mara kadhaa. Vilevile ugonjwa wa Sele umesimuliwa mara nyingi katika hadithi. Pia kulazwa kwa Sele hospitalini kulitokea mara moja (uk.52-62) lakini kulisimuliwa tena mara ya pili na Jamila akiwaelezea akina Bi. Rahma na Zainabu. Anasema "...Hata alipokuja hospitalini hali yake ilikuwa hivi hivi." (uk.88).

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* ukosefu wa dawa hospitalini, umaskini na vifo vya watoto vimesimuliwa mara kadhaa katika matini. Vilevile kuja kwa wageni mjini Cheneo, tukio lililotokea mara moja, lakini kumesimuliwa mara kadhaa katika hadithi nzima.

### 2.3.3 Usimulizi Banifu

Katika aina hii ya usimulizi tukio linaweza kutokea mara kadhaa na kusimuliwa mara moja katika matini. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* Zainabu anatueleza kuwa Aisha huandaa biriani, hii ina maana ya kuwa ameshaandaa biriani sio mara moja wala mbili bali ni mara kadhaa. Anasema:

> **Zainabu:** Hilo hatujalisahau. Aisha huandaa biriani akiwa na muda wakutosha. Mara nyingine wali mweupe, mara nyingine pilau au hata chapati... (uk.15)

Mofu 'hu' katika kitenzi 'huandaa' inarejelea hali ya mazoea. Hii ina maana kuwa Aisha anapika biriani mara kwa mara lakini katika simulizi tendo hilo la mara kwa mara limesimuliwa mara moja.

Pia usimulizi wa aina hii umejitokeza katika *Kijiba cha Moyo* kupitia usemi wa Sele. Anasema, "Ameniambia mara kadha sasa. Kila akija anataka kujua lini hili litafanyika." (uk.36). Mara kadha inamaanisha kuwa tendo hilo limetokea mara nyingi. Kupitia usemi huu tunafahamu kuwa daktari amekuja kwa Sele mara nyingi kumuuliza juu ya *plastic surgery*.

Usimulizi wa aina hii vilevile umejitoza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Mathalan, daktari Siki anaposema, "Si neno lakini kwa nini kila mara sisi tujilinganishe na majirani dhaifu?" (uk.11). Kila mara hapa ina maana kuwa sio mara moja au mbili bali mara nyingi Wanacheneo wamejilinganisha na majirani wao dhaifu.

Usimulizi banifu pia unajitokeza katika tamthilia ya *Kijiba cha Moy*o pale ambapo Sele anasema, "...Nyinyi ndio hamtaki kunielewa. Mnanichukulia kama mtoto. Nimewaambia mara nyingi kuwa sitaki..." (uk.11). Hii ina maana kuwa Sele ameshawaambia mara zaidi ya moja na hii haikuwa mara ya kwanza kuwaambia. Hii inadhihirika kupita matumizi ya maneno "mara nyingi." Usimulizi banifu pia umedhihirika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kupitia dondoo hii:

| | |
|---|---|
| **Waridi:** | Lilikuwa jambo la kusikitisha kumtazama mtoto wa mama mdogo akifia mikononi mwangu naye amenitazama kuokoa maisha ya bwana mdogo. Haikuwa rahisi kwetu sote. |
| **Siki:** | (*Anatikisa kichwa kukubaliana naye. Kisha kwa unyonge anazungumza*). Binafsi yamenipata mara nyingi. Yataka sana moyo! (uk.36) |

Kwa kutumia maneno, “mara nyingi” daktari Siki anamaanisha kuwa yaliyomfika nesi Waridi ya kupoteza jamaa yake, yeye pia yamemfika sio mara moja. Matukio hayo yamesimuliwa mara moja tu katika hadithi.

**Hitimisho**

Sura hii imechunguza kipengele cha wakati na vipengele vyake. Katika kuviangalia vipengele hivi, tumeona jinsi dhana ya wakati ilivyo muhimu katika utanzu wa tamthilia kama ilivyo katika tanzu nyingine za nathari. Imedhihirika kwamba kazi yoyote ya kidrama huhusisha suala la wakati.

Kipengele cha mpangilio kimedhihirika katika tamthilia zinazochunguzwa kupitia mazungumzo ya wahusika kwa kutumia mbinu ya analepsia na prolepsia. Kupitia analepsia tumeweza kufahamu matukio yaliyotokea kabla ya hadithi kuanza na hivyo kutusaidia kuifahamu vyema hadithi. Kupitia prolepsia tumeweza kufahamu matukio kabla muda wake wa kutokea. Prolepsia zimechukua nafasi ya taharuki.

Vilevile, kupitia matini elekezi na mazungumzo ya wahusika katika tamthilia zote mbili kipengele cha muda kimedhihirika ambacho kimetusaidia kuelewa muda uliochukuliwa na hadithi pamoja na kasi ya usimulizi. Tumepata kuona matumizi ya muhtasari, mtuo, onyesho na udondoshi. Kipengele cha idadi marudio pia kimedhihirika katika tamthilia zote mbili. Tumegundua kwamba katika tamthilia zote mbili, kuna usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu.

## SURA YA TATU

## DARAJA NA SAUTI ZA USIMULIZI


### 3.0 UTANGULIZI

Usimulizi wa hadithi unaweza kutokea katika daraja mbalimbali. Katika ploti kuu, mwandishi anaweza kuingiza hadithi zingine fupi zikielezwa na wasimulizi wengine kutoka mwelekeo mwengine tofauti na ule wa ploti kuu. Yaani kunaweza kuwa na hadithi ndani ya hadithi kuu na hadithi nyingine ndani ya hadithi hiyo inayoibuka katika hadithi kuu.


Dhana hii ya daraja za usimulizi imeshadidiwa na Rimmon-Kenan (1983) aliyesema, katika hadithi kunaweza pia kuwa na usimulizi wa hadithi. Mhusika anayesimuliwa katika hadithi kuu anaweza kusimulia hadithi nyingine na ndani ya hadithi yake mnaweza kuwa na mhusika anayesimulia hadithi nyengine na ikaendelea vivyo hivyo hadi mwisho.

Simulizi hizi ndani ya simulizi nyengine ndizo zinazounda vidaraja vya usimulizi. Kila simulizi iliyomo ndani ya nyengine huitegemea simulizi ambamo imetegemezwa. Dhana hii, Genette (1980) ameielezea kwa kutumia mchoro wa vibonzo, vilevile inaweza kuelezwa kwa kutumia maboksi ya Kichina (*Chinese boxes*) kama ifuatavyo:

**(a) Mchoro a** **(b) Mchoro b**




a.




b .

Katika mchoro (a), hadithi kuu ni A na hadithi tegemezwa ni B. Katika mchoro (b) hadithi kuu A imetegemezewa hadithi mbili B1 na B2 na ndani ya hadithi B2 kumetegemezwa hadithi nyengine C.

### 3.1 Aina za Daraja zaUsimulizi

Genette (1980) ameainisha aina tatu za daraja za simulizi, daraja ya kwanza ameiita *Extradiegetic* ambayo ndiyo hadithi msingi, daraja ya pili ni *intradiegetic* ambayo ndiyo hadithi kuu inayotukia katika hadithi msingi na daraja ya tatu ni *Metadiegetic* ambayo imeegemezwa katika daraja ya pili.

#### 3.1.1 Daraja ya Kwanza

Usimulizi wa hadithi kuu hutokea katika daraja ya kwanza. Daraja hii huwa juu ya hadithi kuu na huhusika na usimulizi wake. Ni katika daraja hii ambamo wasimulizi wa tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* wanasimulia hadithi kuu zilizomo katika tamthilia hizo.

Hadithi kuu katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ni kuhusu ugonjwa wa Sele, fadhaa na mahangaiko wanayoyapitia jamaa zake na hatimaye ufumbuzi wa kinachomsumbua Sele. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, hadithi kuu ni kuhusu utepetevu wa baraza la manispaa ya Cheneo unaowasilishwa kupitia Meya na madiwani wake. Hadithi pia inasimulia athari za utepetevu huo wa Meya na madiwani wake, ambazo ni migomo ya wafanyakazi, kutapakaa kwa uchafu, vifo na njaa miongoni mwa wanacheneo.

#### 3.1.2 Daraja ya Pili

Hii ni daraja iliopo chini kidogo baada ya daraja ya kwanza. Inahusu matukio yanayosimuliwa na daraja ya kwanza. Hii ndiyo hadithi kuu. Matukio yote yanayotokea katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* yamo katika daraja ya pili. Kwa mfano, tukio la Sele na Aisha kucheza muziki, Bi. Rahma

kumtembelea Zainabu nyumbani kwake na kadhalika, yote haya ni matukio katika daraja ya pili.

### 3.1.3 Daraja ya Tatu

Hadithi zinazosimuliwa na wahusika katika daraja ya pili huingia katika daraja ya tatu. Usimulizi wa hadithi huwa umo katika daraja ya pili lakini matukio yanayosimuliwa huwa katika daraja la tatu. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* kuna usimulizi wa daraja ya tatu. Usimulizi huu umewasilishwa kupitia Sele pale anapomsimulia Aisha hadithi ya papa na vidagaa (uk.37-39). Hadithi ya papa na vidagaa inasimuliwa na Sele ambaye ni mhusika katika hadithi ya daraja ya pili.

Vilevile hadithi ya daktari mrefu, daktari mfupi na mganga katika *Kijiba cha Moyo* (uk79-81) ni hadithi tegemezi ambayo Sele anamsimulia Zainabu. Hii ni ndoto kwa sababu katika uhalisia mtu hawezi kutapika moyo wake na aendelee kuishi. Hata Zainabu anaitilia shaka kuwa hii ni ndoto tu anaposema, "Mwanangu, labda hiyo ni ndoto tu." Naye Sele anakiri ni ndoto lakini anasisitiza kuwa mna ukweli fulani katika ndoto yake. Anasema, "Basi hiyo jana wamekuja wote watatu. Mimi nimelala chumbani." Hii ina maana Sele alikuwa usingizini. Anaendelea kusema, "Hata ndoto ni nusu ya ukweli. Huwezi kuota kisichokuwepo." Hii ina maana ameota na anaamini ndoto yake. Hivyo basi, hii ndoto inakuwa katika daraja ya tatu ya usimulizi.

## 3.2 Dhima za Hadithi Tegemezi katika Kijiba cha Moyo na Mstahiki Meya

Hadithi tegemezi huweza kuwa na dhima mbalimbli ndani ya hadithi ambamo zimetegemezwa. Huweza kutekeleza jukumu moja au hata zaidi ya moja. Hadithi tegemezi huweza kuwa na jukumu la kiutekelezaji, kiufafanuzi na kimaudhui.

### 3.2.1 Dhima ya Kiutekelezaji

Hadithi tegemezi inaweza kutumika kusukuma mbele hadithi. Rimmon-Kenan (1983) amepeana mfano wa hadithi za Scheherezade katika simulizi ya *A Thousand and One*

*Nights* kama unaodhihirisha jukumu hili. Maisha ya Scheherezade yalitegemea uwezo wake wa kumteka bakunja sultan kupitia usimulizi wa hadithi. Kwa kutegemeza vijihadithi vingi katika hadithi yake aliweza kuepuka kuuliwa na sultan. Hadithi za Sele katika *Kijiba cha Moyo* kama vile hadithi ya papa na vidagaa (uk.36-39), na hadithi ya madaktari na mganga (uk.79-81) zimetekeleza mbali na majukumu mengine kusukuma mbele hadithi.

### 3.2.2 Dhima ya Kiufafanuzi

Hadithi tegemezi inaweza kutumiwa kufafanua matukio yaliyopelekea kuwepo na hali fulani katika hadithi ambamo imetegemezwa. Mfano mzuri ni analepsia. Kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mchezo wa Dida umetumika ili kufafanua yaliyojiri wakati wa mgomo wa wafanyakazi. Mgomo wenyewe haukusimuliwa wakati ukifanyika, tumekuja kufafanuliwa yaliyojiri wakati wa mgomo huu kupitia analepsia. Pengo hili limekuja kujazwa na hadithi tegemezi.

Hadithi ya papa na vidagaa katika *Kijiba cha Moyo*, imetumika kufafanua maisha halisi yalivyo katika ulimwengu wa kihadithi. Ambapo wenye vyeo na mamlaka wanawagandamiza wanyonge. Nao wanyonge licha ya kudhulumiwa na wenye vyeo bado wangali wanawategemea hao hao. Tunaelezwa, “...Mwili wake una uwezo wa kuzuia mawimbi ya bahari navyo vidagaa hujificha nyuma yake kujisitiri. Vidagaa vinajua ni hatari lakini afadhali hatari ya papa kuvila...” (uk.37). Hali hii ndiyo iliyompelekea Sele kutafakari upya juu ya uhusiano wao na wafadhili wao na hiki ndicho kijiba katika moyo wa Sele. Kijiba hiki ndicho kinachomfanya kudhaniwa kwamba yeye ni mgonjwa.

### 3.2.3 Dhima ya Kimaudhui

Uhusiano uliopo kati ya hadithi msingi na hadithi tegemezi ni wa kianalojia. Kwa mfano hadithi ya Sele ya madaktari na mganga katika tamthilia ya *Kijiba cha moyo* ni sitiari ya maisha yalivyo katika ulimwengu wa kihadithi (ulimwengu wa hadithi kuu) ambamo hadithi imeegemezwa. Daktari mrefu anawakilisha nchi za magharibi (Waingereza), naye daktari mfupi mwenye misuli anawakilisha nchi za mashariki

(China), mganga mwenye viguo vilivyoparara na kumbana na kibuyu cha dawa mkononi anawakilisha nchi za bara la Afrika na Sele vilevile akiwakilisha nchi ya Kiafrika.

Kule kuja kwa daktari mrefu akifuatiwa na daktari mfupi na nyuma yao wakifuatiwa na mganga wakati Sele amelala inaashiria majio ya wakoloni wakati Waafrika wenyewe hawatambui. Kujibizana kwa furaha na kukumbatiana na kisha kuzozana kwa madaktari wakiwa karibu na Sele kunaashiria kutoafikiana kwao kuhusu ugawaji wa rasilimali kutoka kwa nchiya Kiafrika (Sele) iliyokuwa bado imelala mbele yao. Wakati wote huu nchi zingine za Afrika (mganga) zilikuwa kando zikitazama.

Tendo la madaktari la kumzungukazunguka Sele, mara wakishauriana na kumuashiria kisha kusema kwa pamoja, “Bado amelala” na kumpekuapekua kila mahali na walipokosa chochote wakaamua kugawana. Tunaelezwa:

> …Waliposhindwa kupata chochote nikaona wamechukua vyembe vyao. Niliogopa. Wazo likanijia la kuwatapikia moyo wangu. Palepale nikautapika. Wote wakaukimbilia. Niliutazama nikaona unafanana na kidagaa cheusi. Wakakitwaa huku wakipigania. Nikajua hawakuja kunitibu mwili wangu bali kuutwaa moyo wangu. Nikapatwa na huzuni. (uk.80)

Dondoo hii inaashiria namna wakoloni walivyokuja bara la Afrika wakachunguza rasilimali zilizoko na wakaona bado Waafrika ‘wamelala’ na hivyo kuamua kutwaa rasilimali hiyo ili kujigawia. Sele kuona hivyo akawatapikia moyo wake. Moyo wa Sele unaweza kuwakilisha madini yanayopatikana ndani ya ardhi. Wakoloni walipopata walichokijia hawakuijali tena nchi ya Kiafrika.

### 3.3 Metalepsia

Hapa ni pale ambapo usimulizi unatoka kutoka kiwango kimoja hadi kiwango kingine cha hadithi. Wakati mkondo wa hadithi unabadilika msimuliwa anaweza kujulishwa

kuwa usimulizi wa hadithi nyengine unataka kuanza au kuisha. Wakati mwengine mkondo wa hadithi unabadilika bila msimuliwa kujulishwa.

### 3.3.1 Badiliko la Usimulizi LililoWazi

Hapa ni pale ambapo msimuliwa anajulishwa kuwa usimulizi wa hadithi nyengine unataka kuanza au kuisha.Kwa mfano katika *Kijiba cha Moyo* daraja ya usimulizi inabadilika kutoka daraja ya pili hadi ya tatu pale Amri anamsimulia Sele hadithi ya lumbwi. Amri na Sele wamo katika hadithi ya daraja ya pili na lumbwi yumo katika daraja ya tatu. Amri anatambulisha mwanzo wa hadithi yake. Anasema:

| | |
|---|---|
| **Amri:** | Unajua kwamba hata lumbwi ana wenyewe-wenyewe? |
| **Sele:** | (*Kimya*) Labda anao lakini wenyewe huo utafaa nini? Dhaifu! |
| **Amri:** | Ungekuwa dhaifu asingekuwa nao wala asingekuwepo lumbwi. Udhaifu huo ndio kinga yake. Na yatosha. Anauamini na kuutegemea. |
| **Sele:** | Alaa! |
| **Amri:** | (*Anacheka kicheko kirefu*.) usimwone yuatembea vile. Eti taratibu. Mwenyewe ana wenyewe-wenyewe wa rangi. Vilevile ana wenyewe-wenyewe wa macho. Dira kamili... (uk.67) |

Hapa Amri ametanguliza usimulizi wa hadithi ya lumbwi kwa swali kisha akaanza kusimulia lumbwi na wenyewe-wenyewe wake. Ingawaje mwisho wa hadithi haujatambulishwa usimulizi unarudi katika daraja ya pili.

Mchezo wa Dida katika *Mstahiki Meya* umeweza kutambulishwa kabla ya kuanza. Msimulizi anatueleza: “Anaigiza sasa” (uk.64). Hii inaashiria kubadilika kwa kiwango cha daraja ya usimulizi. Dida yumo katika daraja ya pili na mhusika askari aliyemo katika mchezo wake yumo katika daraja ya tatu.

Hali hii inadhihirika kwa uwazi zaidi hasa pale kuna mtambaji wa hadithi. Mfano mzuri wa kutambulishwa kwa kubadilika daraja ya usimulizi unapatikana katika tamthilia ya *Lina Ubani* ya Muhando kabla ya usimulizi wa hadithi ya Bibi ya Dyamini inayosimuliwa na Mtambaji. Tunaelezwa:

**Mtambaji:** Kwa nia moja
Mawingu kutaka angusha Bibi hadithi
Akaitamba.
Akaitamba ikatambika
Mimi si hodari kama yeye
Lakini hadithi hiyo takutambieni
Palitokeani
Hapo zamani za kale
Palitokea kijiji kimoja
Jina Bibi hakutaja
Kijiji chenye neema
Watu wake wengi wema
Kazi wakizichapa kwa bidii na vicheko
Hakika walineemeka.
Lakini penye wema ubaya huzengeya
Katokea zimwi
Katokea atokako.... (uk.18)

Badiliko katika utambaji wa hadithi limetambulishwa na Mtambaji ambaye ni mhusika katika daraja ya pili na hadithi ya Dyamini iko katika daraja ya tatu.

### 3.3.2 Badiliko la Usimulizi Lisilo Wazi

Hapa ni pale ambapo usimulizi wa hadithi unabadilika bila msimuliwa kujulishwa. Kwa masimulizi ya Bi.Rahma kuhusu pepo katika *Kijiba cha Moyo* (uk.40) hayakutambulishwa yalipoanza. Msomaji anaweza asitambue kuwa daraja ya usimulizi imebadilika.

### 3.4 Uhusiano wa Kiwakati baina ya Usimulizi na Hadithi

Kulingana na Genette (1980) uhusiano wa kiwakati uliopo baina ya usimulizi na hadithi ni wa aina nne: usimulizi wa kiurejeshi (*ulterior*) usimulizi tangulizi (*anterior*) na usimulizi sawia (*simultaneous*) na usimulizi wa kimpishano (*intercalated* ).

#### 3.4.1 Usimulizi wa Kiurejeshi

Huu ni usimulizi wa matukio baada ya kutokea kwake. Usimulizi huu hutambulishwa na matumizi ya kiambishi cha wakati uliopita 'li'. Mfano wa usimulizi wa aina hii umejitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* pale Beka anapozungumza katika kikao na Meya. Anasema, "Hata hapo zamani tulipopata ilikuwa ni vipeni viwili vitatu ilhali nyinyi mlipata nyongeza kubwa... (uk. 68). Vilevile usimulizi wa kiurejeshi unaweza kutambulishwa kwa kutumia kiambishi cha hali timilifu 'me'. Kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Beka anasema:

**Beka:** (*Kwa uchungu.*) Juzi mtoto wa Kerekecha amekufa kama nzi. Amemfia mikononi mwake mwenyewe Kerekecha akitazama... (uk.69)

Katika mfano huu wa pili kiambishi 'me' kinawakilisha wakati uliopita. Hii ina maana kuwa matukio yanayosimuliwa yamekwisha kufanyika.

#### 3.4.2 Usimulizi Tangulizi

Huu ni usimulizi ambao unatangulia wakati wa matukio yanayosimuliwa. Usimulizi huu aghalabu hautumiki sana. Rimmon- Kenan (1983) anasema, usimulizi huu ni wa kitabiri, na hasa unatumia njeo ijayo. Katika tamthilia zinazochunguzwa usimulizi huu umetumika kwa kiwango kidogo. Usimulizi huu umedhihirika kupitia matumizi ya prolepsia. Kwa mfano:

**Meya:** Mara hii sitaki kusikia mtu amekufa. Mwaka wa kuomba kura <u>utakapofika</u> sitataka

mizuka yao kuniandama. Itaniletea tatizo wakati wa uchaguzi.

**Diwani I:** Nitawaambia kutembeza virungu kiasi cha kuwafanya kutulia nyumbani. (uk.19)

Katika mfano huo tunaona matumizi ya kiambishi cha wakati ujao 'ta' kimetumika. Hii ina maana kuwa matukio yanayosimuliwa hayajatokea.

### 3.4.3 Usimulizi Sawia

Hii ni aina ya usimulizi ambao huwa sawia na matukio yanayosimuliwa. Yaani matendo yanatokea wakati huo huo wa usimulizi. Usimulizi huu ndio uliotamalaki katika tamthilia zote mbili. Kwa mfano tunaelezwa:

> (Meya anayaweka mafaili pembeni. Anainuka. Anatazama nje kupitia dirishani. Anatikisa kichwa. Anarudi kuketi. Anachukua gazeti lililo mezani na kuanza kusoma. Sauti ya kiongozi wa wafanyakazi inasikika kupitia kwa kipaza sauti.)
>
> **Sauti:** Ndugu wafanyakazi wenzangu... (uk.57)

Katika mfano huu kutoka *Mstahiki Meya* tunaona matukio yakitendeka wakati huo huo yanaposimuliwa hivi kwamba tunaweza kupata picha kamili ya yanayofanyika.

## 3.5 Aina za Wasimulizi

Katika usimulizi wowote huwa kuna sauti inayoelezea au kuyasimulia matukio yanayotokea au kupatikana hadithini. Sauti hiyo inatokana na msimulizi. Rimmon-Kenan (1983) anapinga mawazo ya Chatman (1978) kuhusu wasimulizi na wasimuliwa. Kwake hawa sio muhimu katika mawasiliano. Anasema kila matini huwa na mtunzi wa kidhahania na msomaji kidhahania lakini msimulizi na wasimuliwa si lazima. Kwa maoni yangu, hakuna usimulizi bila msimulizi wala wasimuliwa. Ndio maana ni muhimu kuangazia aina za wasimulizi na wasimuliwa.

Kimsingi, kuna maswali kadhaa ambayo huiweka wazi zaidi mbinu iliyotumika katika usimulizi. Ni vyema kuelewa ni nani anayeisimulia kazi hiyo na ana uhusiano gani na matukio ya hadithi husika? Jambo la muhimu katika swali hili ni uelewaji wa uhusika wa msimulizi. Anashiriki katika hayo matukio au la? Hayo ni baadhi tu ya maswala muhimu ambayo humsaidia msomaji wa kazi hiyo kuelewa msimulizi wake pamoja na mchango wake katika kuikamilisha. Katika kuainisha wasimulizi, Genette (1980) ametumia vigezo viwili muhimu: daraja ya simulizi na uhusiano wa msimulizi na hadithi anayosimulia.

### 3.5.1 Daraja ya Simulizi

Katika kigezo cha daraja ya hadithi anayosimulia msimulizi, tunapata aina mbalimbali za wasimulizi kutegemea kiwango cha hadithi aliomo msimulizi. Kuna wasimulizi wa daraja ya kwanza (*extradiegetic*) na wa daraja ya pili (*intradiegetic*) na hata daraja ya tatu na nne (*metadiegetic/ hypo-diegetic*). Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* zina wasimulizi wa daraja ya kwanza na ya pili pekee.

Msimulizi wa daraja ya kwanza, huyu ni msimulizi anayesimulia hadithi inayopatikana katika daraja ya pili. Msimulizi wa aina hii amedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* ambapo sauti yake inasikika kupitia matini elekezi. Aghalabu anatumia usimulizi wa nafsi ya tatu ambao unatambulishwa na matumizi ya mofu ‘a’. Kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* tunapata usimulizi ufuatao:

> Jioni. Zahanatini. Daktari Siki katika mavazi yake rasmi anaonekana mwenye wasiwasi. Anaranda kutoka sehemu moja ya chumba huku akikagua visaraka kadhaa kabla ya kusita. Anashika kiuno kwa mikono yake miwili. Anatikisa kichwa kama asiyekubaliana na jambo fulani. Anaketi kwenye kiti nyuma ya meza. Muda wote huu kuna milio ya watoto inayosikika kwa mbali. (uk.1)

Anayesimulia yuko katika daraja ya juu kuliko hadithi yenyewe (yuko katika daraja ya kwanza). Yeye si mhusika katika simulizi yake, anatusimulia juu ya daktari Siki ambaye ni mhusika katika hadithi kuu (daraja ya pili).

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* maelezo juu ya mazingira na anachokifanya Sele ni mfano wa usimulizi wa daraja ya kwanza. Kwa mfano:

> Nyumbani kwa Sele. Siku hiyo alasiri. Onyesho linapoanza tunamkuta Sele ameketi ukumbini. Ameshika tama akiwa katika hali ya kujiinamia. Anatikisa kichwa mara kama anayekubaliana na jambo na mara kama mwenye kukataa. Kwa mbali unasikika mlio mseto wa ngoma na piano. Katika baadhi ya sehemu mlio wa ngoma unazidi ule wa piano na katika nyengine ule wa piano unazidi ule wa ngoma, hata hivyo hazifuati mahadhi mbalimbali. Zainabu na Bi.Rahma wanapoingia wanamkuta Sele katika hali ya kujiinamia. (uk.40)

Sauti inayosikika ni ya msimulizi. Hayumo katika hadithi anayoisimulia, anasimulia kwa kutoka nje. Anatumia usimulizi wa nafsi ya tatu. Matukio kuhusu Sele, Zainabu na Bi.Rahma yamo katika hadithi kuu.

Vilevile kuna msimulizi wa daraja ya pili. Huyu ni msimulizi ambaye ni mhusika katika daraja ya pili. Hadithi anayosimulia msimulizi wa daraja ya pili huwa katika daraja ya tatu. Kwa mfano Dida katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, anaigiza yaliyotokea katika mgomo wa wafanyakazi. Anasema:

> (*Anaigiza sasa*.)
> Bunduki inayotoa risasi tatu tatu
> basi tena umelala chini hivi.
> (*Anaonyesha kwa vitendo kisha anainuka*.)
> Mlio wake
> Vitoa machozi
> Magari yanayotapika maji.

(*anacheka kicheko kirefu*.)
Wakati wa mauti kama juzi
Kumbe wazee huwashinda mbio vijana!
Roho ya mtu hapendi mtu imponyoke.
Kwa bahati mbaya ikiponyoka
Wakubwa hueleza haikutoka.
(*Anacheka kicheko kirefu*.)
(uk.64-65)

Kupitia maigizo ya Dida tunapata hadithi ya yale yaliyotokea wakati wa mgomo wa wafanyakazi. Ambapo anatueleza kuwa kulikuwa na askari waliowafyatulia risasi waliogoma na pia kuwatupia vitoa machozi na kuwamwagia maji. Anatueleza pia kulikuwa na tafrani ambapo kila mtu alikuwa akikimbilia maisha yake. Ambao hawakubahatika walifariki na viongozi hawakujali. Dida ni mhusika katika daraja ya pili na anacheza nafasi ya askari katika mchezo ndani ya mchezo anaotusimulia. Hivyo basi kumfanya Dida kuwa msimulizi wa daraja ya pili.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, Sele anajitokeza wakati mwengine kama msimulizi wa daraja ya pili pale ambapo anasimulia hadithi. Kwa mfano hadithi ya papa na vidagaa. (uk.36-39)

### 3.5.2 Uhusiano wa Msimulizi na Hadithi

Msimulizi yeyote wa daraja ya kwanza na pili au hata tatu anaweza kuwa mhusika katika hadithi anayoisimulia au hata asiwe mhusika katika hadithi. Tunapata msimulizi tawasifu (*homodiegetic*) na msimulizi wasifu (*heterodiegetic*).

#### 3.5.2.1 Msimulizi Tawasifu

Huyu ni msimulizi ambaye anapatikana katika hadithi anayosimulia na hadithi inamuhusu. Kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, daktari Siki anamsimulia Diwani III namna watoto wanavyofia mikononi mwa wazazi wao na mwa matabibu hali anawaangalia. Anasema:

> **Siki:** ...Watu wananijia hospitalini kwa kutumainia kuwa nitawasaidia. Ninatazama watoto wakifia mikononi mwa wazazi wao na wakati mwengine mwa matabibu kwa kukosa dawa ilhali hawa ni wafanyakazi wa mji wa Cheneo. Dawa hakuna... (uk.46)

Kupitia maelezo haya tunapata kufahamishwa hali ilivyo mbaya hospitalini ambako watoto wanakufa mikononi mwa wazazi wao kwa kukosa dawa. Vilevile Sele katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* anajitokeza kama mhusika tawasifu katika hadithi yake anayomsimulia Zainabu juu ya madaktari na mganga ambamo yeye mwenyewe ni mhusika (uk.79-81).

### 3.5.2.2 Msimulizi Wasifu

Huyu ni msimulizi ambaye hayumo katika hadithi anayosimulia. Kwa mfano msimulizi anaweza kusimulia matukio ya mhusika au wahusika wengine. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* msimulizi anatueleza:

> (*Zimepita siku mbili. Nyumbani kwa Meya. Dida*
>
> *anafagia. Ghafla anakumbuka kitu na kuanza kucheka; kicheko kirefu.*)
>
> **Dida:** Duniani kuna watu na viatu
>
> na Cheneo ina watu na viatu.
>
> (*Anachekakicheko kirefu*.)
>
> Paka na panya
>
> Panya na paka!
>
> (*Anachekakicheko kirefu tena.*)
>
> *Kisha anapiga kwata kama askari*.)
>
> (*Anauchukua ufagio kuwa bunduki*.)
>
> Let rat! Let rat! Let rat! Let rat!
>
> (*Anapofika mwishoni mwa chumba anasimama. Anageuka kama askari katika kwata na kupiga saluti. Kinafuata kicheko chake kirefu*.)... (uk.64)

Katika dondoo hii, kuna masimulizi na hadithi inayosimuliwa. Maelezo yaliyomo katika hati za italiki ni masimulizi na maandishi yaliyo wima ni hadithi inayosimuliwa. Msimulizi yuko nje ya hadithi anayosimulia. Msimulizi huyu ni wa daraja ya kwanza na ni msimulizi wasifu (*extra-heterodiegetic*.) Dida katika hadithi hii ni msimulizi wa daraja ya pili na ni mhusika wasifu vilevile (*intra-heterodiegetic*.)

### 3.5.3 Utambulisho wa Msimulizi

Msimulizi anayepatikana katika simulizi anaweza kutambulishwa (*overt*) au asitambulishwe (*covert*). Msimulizi katika tamthilia zote mbili za *Mstahiki Meya* na *Kijiba cha Moyo* anaweza kutambulika. Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (1983) kuna ishara nyingi zenye kumtambulisha msimulizi katika matini. Ishara zenyewe ni kama vile: maelezo ya mandhari, kutambulisha wahusika, kutoa muhtasari wa muda, kueleza wahusika, kueleza jambo ambalo mhusika hakusema au fikiria na kutoa maoni.

#### 3.5.3.1 Maelezo ya Mandhari

Malezo ya Mandhari yanaashiria kuwepo kwa msimulizi kwa mfano katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* tunaelezwa:

> Siku kadhaa zimepita. Ni adhuhuri. Sele yumo katika chumba cha kulala. Yuko mbele ya kioo. (uk.31).

Maelezo haya yanaashiria kuwa yupo mwenye kuyasimulia ambaye ni msimulizi. Mahali pa matukio ni katika chumba cha kulala cha Sele. Vilevile hali hii imedhihirika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kama ifuatayo:

> Katika ofisi ya siku. Siki ameketi akisoma gazeti.
>
> Kuna koti jeupe la kazi lilikunjwa vizuri kando ya meza... (uk.34)

Maelezo hata vilevile yanatolewa na msimulizi wa daraja ya kwanza. Msimulizi anatambulishwa kwa matumizi ya kiambishi cha nafsi ya tatu ‘a’ cha usimulizi wa nafsi ya tatu.

### 3.5.3.2 Kutambulisha Wahusika

Katika tamthilia zote mbili, wahusika wametambulishwa kwa msomaji mwanzoni mwa matini. Wahusika hawa wametambulishwa kwetu na msimulizi. Hivyo basi kudhihirisha kuwepo kwake katika matini. Kwa mfano wahusika katika *Mstahiki Meya* wametambulishwa kama ifuatavyo:

Meya - Meya wa Baraza la Mji.

Gedi - Mpambe wa Meya.

Dida - Mhudumu wa nyumbani kwake Meya.

Bili - Rafiki yake Meya.

Siki - Daktari.

Waridi - Nesi.

Mama - Mfanyakazi wa Baraza la Mji.

Diwani I

Diwani II } Wanakamati wa Kamati ya Meya.

Diwani III

Mhubiri

Tatu

Beka } Wawakilishi wa wafanyakazi.

Medi

Askari I Polisi.

Askari II Polisi.

Sauti Sauti za Wafanyakazi.

Wahusika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* pia wametambulishwa kwa msomaji mwanzoni mwa hadithi ifuatavyo:

Sele - Mumewe Aisha (Miaka 30)

Aisha - Mkewe Sele (Miaka 25)

Zainabu - Mamake Sele

Musa - Babake Sele

Amri - Babu yake Sele

Bi. Rahma- Shangaziye Zainabu

Daktari - Tabibu wa Sele

Jamila – Kijana muuguzi wa kijijini mwao Sele.

Maelezo yote hayo juu ya majina na maelezo kuhusu wahusika yametolewa na msimulizi. Hivyo basi kudhihirisha kuwepo kwake katika hadithi.

#### 3.5.3.3 Muhtasari wa Muda

Sauti ya msimulizi inasikika pale anapotupatia muhtasari wa muda ambao umepita katika hadithi. Kwa mfano katika kila mwanzo wa onyesho tunapata maelezo juu ya muda. Mfano, "Siku ya pili alasiri. Nyumbani kwa Diwani III..." (*Mstahiki Meya* uk. 45). Maelezo haya yanadhihirisha kuwepo kwa msimulizi.

### 3.6 Wasimuliwa

Kwa mujibu wa Genette (1980) msimuliwa huwa katika daraja sawa na msimulizi. Hivi ni kusema kuwa kila msimulizi huwa na msimuliwa au wasimuliwa wake anaowalenga. Vigezo vinavyotumika kuainisha wasimulizi pia vinaweza kutumika kuainisha wasimuliwa.

### 3.6.1 Kigezo cha Daraja ya Usimulizi

Kwa kutumia daraja ya usimulizi kama kigezo cha kuainisha wasimuliwa tunaweza kutofautisha msimuliwa aliye 'juu' kuliko hadithi (*extradiegetic*) yaani msimuliwa wa daraja ya kwanza na msimuliwa wa daraja ya pili, ambaye yumo ndani ya hadithi kuu (*intradiegetic*).

Kwa mfano msimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* anawasimulia wasomaji walio katika daraja ya juu kuliko hadithi inayosimuliwa. Hivyo basi wasomaji wanakuwa katika daraja ya kwanza. Msimulizi wa daraja ya kwanza anasimulia kupitia maandishi ya mlazo.

Wasimuliwa walio ndani ya hadithi kuu (daraja ya pili) husimuliwa na msimulizi wa daraja ya pili vilevile. Wasimuliwa na msimulizi wote huwa ni wahusika katika hadithi inayosimuliwa na msimulizi wa daraja ya kwanza. Tamthilia zote mbili zimesheheni mifano ya wasimuliwa wa daraja ya pili. Kwa mfano katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, Bi. Rahma anamsimulia Zainabu kuhusu pepo. Anasema, "Pepo. Nakumbuka zamani tuliambiwa kuhusu pepo kuwapagawa watu na kuteka nyoyo zao...." (uk.40-41). Msimuliwa wa daraja ya pili hapa ni Zainabu.

### 3.6.2 Kigezo cha Ushiriki katika hadithi

Kwa kutumia kigezo hiki tunaweza kutofautisha wasimulizi wanaoshiriki katika hadithi wanayosimuliwa na wale ambao hawashiriki katika usimulizi. Kama ilivyo katika kuwaainisha wasimulizi, wasimuliwa vilevile wanaweza kutambulika (*overt*) au wasitambulike (*covert*) katika usimulizi. Wasimuliwa wanaweza kutambulishwa na msimulizi kupitia kukisia majibu yao au kupitia majibu yao wenyewe, maoni yao au hata vitendo (mfano kupiga makofi) katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* aina zote mbili za wasimuliwa zimedhihirika. Kwa mfano:

**Aisha:** Kila wakati unaniambia wanavyohangaisha vidagaa lakini hujawahi kuniambia kuwa hupigana wao kwa wao.

**Sele:** (*Amehamasika*) Kupigana Papa hupigana.
Tena papa wenyewe wengi. Wakati mwingine hupigana hadi kuuana. Vita vyao si mchezo. (*Kimya*) vinatisha. Papa akilemea papa mwenzake humuumiza vibaya. (uk. 36)

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, wasimuliwa wanaweza kuonekana wazi kwa mfano sauti inasema:

**Sauti:** Ndugu wafanyakazi wenzangu.
Tumefika hapa tukiwa kitu kimoja
Na umoja huu ndio nguzo yetu
Tushikamane hadi mwisho
Mwisho wa madhila yanayotuzonga
(*Wafanyakazi wanashangilia*.)
Ndugu zangu katika vita hivi
Msisahau kuwa kwa muda sasa
Tumeonewa vya kutosha
Tumedhalilishwa vya kutosha (uk.57)

Kupitia sauti tunaweza kuwatambua wasimuliwa. Wasimuliwa wametajwa wazi na msimulizi. Wasimuliwa ni wafanyakazi. Vilevile wafanyakazi wametambulishwa kama walengwa wa mazungumzo ya kiongozi wao kwa kupiga makofi.

Mfano wa msimuliwa au wasimuliwa ambao hawashiriki katika usimulizi na wala hawatambuliki ni katika mchezo wa Dida kwenye tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Katika ukurasa 64-65 Dida anazungumza kando lakini wasimuliwa wake sio wazi. Vilevile Meya anapozungumza pekee katika ukurasa wa 57 anasema:

**Meya:** Nalimwambia hakusikia
Msiba wa kujitakia
Kilio kamwe hauna
Mpiga ngumi ukuta

Hujutia kitendo chake. (Uk. 57-58)

Maneno haya ya Meya hayajalengwa mtu mahususi kwani Meya yuko pekee ofisini mwake.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumeshughulikia daraja za usimulizi, dhima za utegemezi, uhusiano baina ya hadithi na usimulizi kiwakati, wasimulizi na aina za wasimuliwa. Imedhihirika kuwa tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* zina usimulizi wa daraja ya kwanza na ya pili. Hivi kwamba utegemezi umeshuhudiwa na mabadiliko kutoka daraja moja ya usimulizi hadi nyengine yametambulishwa.

Aina zote tatu za usimulizi kwa mujibu wa Genette (1980), usimulizi wa matukio yaliyokwisha kutendeka, usimulizi wa matukio yajayo na usimulizi sambamba na matukio umetumika katika tamthilia zote mbili kama tulivyodhihirisha. Aina za wasimulizi zilizodhihirika ni msimulizi wa daraja ya kwanza na ya pili, tawasifu, wasifu na pia msimulizi ameweza kujitokeza wazi (*overt*) katika tamthilia zote mbili. Wasimuliwa ambao wamedhihirika ni wa daraja ya kwanza, pili na wasimuliwa waliotambulishwa.

# SURA YA NNE

## WAHUSIKA NA UHUSIKA

### 4.0 UTANGULIZI

Wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaopatikana katika kazi ya fasihi na wenye sifa za kibinadamu. Aghalabu huwa na sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo), Wamitila (2002).

Msingi wa hadithi yoyote ile ni wahusika ambao hadithi inayosimuliwa huwa inawahusu. Kulingana na Wamitila (2008) wahusika ni jira muhimu katika kazi za kifasihi kwa kuwa huwa watendaji wakuu wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi zenyewe.

Usawiri wa wahusika katika tamthilia mara nyingi hukuzwa katika hali banifu. Aghalabu huwa wachache na huwa hawakuzwi kikamilifu kwa sababu ya kubana kutokana na ‘ufupi’ wa nafasi katika tamthilia. Hii ni kwa sababu tamthilia ni utanzu ulio na sifa ya ubanifu katika uwasilishaji jukwaani. Utafiti huu utachunguza usawiri wa wahusika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*.

### 4.1 Mbinu za Usawiri wa Wahusika

Kama anavyosema Wamitila (2008), wasomaji na wahakiki wa fasihi hutegemea sifa kadha kuwaelewa wahusika: Maumbile yao, mienendo na tabia zao, lugha zao, vionjo vyao, uhusiano wao na wahusika wengine, hisia zao wenyewe, mazingira na mandhari yao, kiwango chao cha elimu, jamii yao na kadhalika.

Mwandishi huwa na uhuru wa kuwateua na kuwawasilisha wahusika. Anaweza kutumia njia mbalimbali katika kuwasawiri wahusika wake. Kwa mujibu wa wananaratolojia kuna njia mbili kuu za kuwasawiri wahusika: usawiri bainishi na usawiri timbe.

### 4.1.1 Usawiri Bainishi

Kupitia mbinu hii, mwandishi au msimulizi hutoa maelezo yanayoifumbata tabia au wasifu wa mhusika moja kwa moja kwa kutumia vivumishi sifa. Matini elekezi ni mbinu ya kisimulizi ambayo mtunzi wa tamthilia anaitumia katika tamthilia, hivyo huwa msingi mkubwa wa kutuelekeza kwenye sifa maalum zinazowahusu wahusika wanaopatikana katika hadithi.

Pili usimulizi unaweza kutokana na mazungumzo ya wahusika. Maoni yanayotolewa na mhusika kuhusu mhusika mwingine yanaweza pia kuangaliwa kama maoni ya kisimulizi, ingawaje kuna tahadhari kwani hayo yanaweza kuwa maoni ya kibinafsi ya huyo mhusika na wala sio sifa bainifu za mhusika anayezungumziwa. Kwa mfano mhusika zuzu anapomuita mwengine 'mwerevu' haimaanishi huyo mhusika anayezungumziwa ni mwerevu. Huenda ikawa kwa maoni ya mhusika zuzu kwake anamuona mwerevu.

Kwa kutumia mbinu hii, mwandishi huwa na nafasi ya kubainisha mapenzi au chuki yake dhidi ya wahusika fulani. Hii ni njia rahisi ya kuwasawiri wahusika na hasa kwa kuwa mwandishi anaweza kutoa maelezo machache yanayoifumbata tabia au wasifu wa mhusika ambao ungechukua muda mrefu kueleweka kutokana na matendo yake mwenyewe. Hata hivyo mbinu hii imebainika kuwa na udhaifu kwa kuwa haimpi msomaji nafasi ya kushiriki katika kutathmini tabia ya mhusika fulani.

Mbinu hii imedhihirika katika tamthilia zinazochunguzwa kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, sifa ya kutoaminika kwa Meya na uaminifu wa Diwani III imesawiriwa kupitia mazungumzo ya daktari Siki anasema:

> **Siki:** …Meya wetu anaweza kusema chochote mradi anaona kuwa kitaonyesha kuwa Baraza inajitahidi kuwajibika. Zake huwa ni kauli zinazoanguliwa katika matamshi. Afadhali Bwana Uchumi na Kazi. Angesema yeye ningeamini. Hadi sasa sijaelewa kwa nini hakujitokeza kueleza hali

> ilivyo badala ya Meya. Huenda hizi ni dalili za mvua. (uk.7)

Kupitia dondoo hii Meya amesawiriwa kama mnafiki asiyetekeleza ahadi hivyo basi kutoaminika, ilhali Diwani III amesawiriwa kama msema kweli na mwenye kutekeleza ahadi zake. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, tunapata sifa ya tabia za Sele kupitia mazungumzo ya Bi. Rahma na Zainabu. Zainabu anasema:

> **Zainabu:** (*Akimwambia Bi.Rahma kando*) Unaona? Hii basi ndiyo hali yake. Huwa kama aliyechanganyikiwa lakini humshindi katika kusema. (uk.40)

Kupitia dondoo hili tunaelezwa tabia ya Sele ya kuchanganyikiwa na mwenye ustadi wa kusema.

### 4.1.2 Usawiri Timbe

Katika mbinu hii uwasilishaji wa wahusika huwa si wa moja kwa moja. Badala ya kutaja tabia za mhusika mbinu hii huidhihirisha na kuitolea mifano kwa njia mbalimbali. Hivi kwamba msomaji huwa na jukumu la kutathmini tabia au wasifu wa mhusika. Njia zinazotumika kudhihirisha tabia ya mhusika ni kama vile, kupitia matendo, usemi, muonekano wa nje, mazingira na majazi.

#### 4.1.2.1 Matendo

Katika mbinu hii usawiri wa wahusika hufanyika kwa kuwaonyesha wakitenda matendo na kumuacha msomaji awaone na kuzichanganua tabia zao kutokana na matendo yao na kufikia uamuzi wake mwenyewe kuwahusu.

Tabia inaweza kudhihirika kupitia matendo ya mara moja na matendo ya mazoea. Matendo ya mara moja na matendo ya mazoea yanaweza kuainishwa katika makundi matatu: tendo la utekelezaji, tendo la kukwepa na tendo la kunuilia.

#### 4.1.2.1.1 Tendo la Utekelezaji

Hili ni tendo linalofanywa na mhusika. Kupitia matendo ya mhusika tunaweza kuthamini tabia zake. Kwa mfano, katika *Kijiba cha Moyo* tunaweza kusema Sele ni mdadisi kutokana na tabia yake ya kuuliza maswali mengi. Alimdadisi daktari alipokwenda hospitalini pia kupitia analepsia tunajuzwa kuwa Sele alimuuliza daktari maswali mengi alipokuja kwao kumtibu. Kwa mfano:

**Sele:** Naelewa lakini nipe nafasi kuuliza swali kabla ya kuanza.

**Daktari:** (*Hana stahamala tena.*) Sitaki maswali yako mengi. Siku ile nyingine umeniuliza maswali mengi ya kunipotezea muda. Mimi ndiye daktari; nakuuliza maswali wajibu. (*Kimya*) wewe ni wa kujibu, Sasa wewe unataka kunihoji na wewe ndiye mhojiwa.

**Sele:** (*Kwa upole*.) Mara hii si mengi daktari.

Kupitia dondoo hii tabia ya Sele ya udadisi inadhihirika kupitia tendo la kuuliza maswali mengi. Anauliza ili apate uhakika kabla ya kufanyiwa upasuaji. Vilevile tabia ya daktari ya kutokuwa na stahamala inadhihirika. Hataki kuulizwa maswali anahisi Sele anampotezea wakati wake bure.

Aisha ni mkewe Sele. Amesawiriwa kama msomi. Sifa hii inadhihirika kupitia tabia yake ya kusomasoma vitabu. Hili linadhihirika kupitia mazungumzo baina ya Aisha, Zainabu na Bi. Rahma kama ifuatavyo:

**Aisha:** Nzuri. Hamna neno. (*Baada ya kumsalimu anaelekea upande ule wa pili wa chumba. Anaanza kuchakura vitabu pembeni. Muda huu wote, wote wawili wamemtazama*.)

**Zainabu:** Aisha!

**Aisha:** Bee! (*Ameinamia rundo la vitabu bado*.)

**Zainabu:** Aisha!

**Aisha:** Bee! (Ameinamia rundo la vitabu bado).

**Zainabu:** Tabia gani hii? Hata kama ulikuwa hapa mapema watoka utokako unafululiza moja kwa moja hadi penye vitabu! Humwoni bibi hapa? Kuna nini.

**Aisha:** (*Akiendelea nashughuli zake*.) Hamna kitu.

**Zainabu:** Hamna kitu?

**Bi. Rahma:** Aisha, desturi gani hii? Mtoto utoke kule nje sisi wazee wako tuko hapa kisha utupuuze na kuelekea kwenye vitabu! Ndiyo elimu yenu hii ya kizungu inavyowatuma kufanya? Huo ndio ustaarabu kwenu? (uk. 18)

Kupitia tendo hilo la Aisha la kuzamia rundo la vitabu kusoma, tunaweza kusema kuwa ni msichana aliyesoma. Pia kupitia tendo hili Aisha amesawiriwa kama mwenye kumjali na kumpenda mumewe na ndiyo maana anasoma vitabu apate kuufahamu ugonjwa wa Sele ili aweze kumwelewa vyema na kumsaidia.

Usawiri wa wahusika kupitia matendo wanayotenda umedhihirika pia katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Kwa mfano daktari Siki amesawiriwa kama mhusika mwenye imani, jasiri na mshauri. Sifa zote hizi zimebainika kupitia matendo yake. Kwa mfano tendo lake la kuwatibu wagonjwa hata kama hawana pesa ni ishara ya imani. Mamake Dadavuo Kaole alipokuja hospitalini na mwanawe kutafuta usaidizi, nesi Waridi alimkaripia kwa kuruka mstari na kumuamuru angoje nje, lakini daktari Siki hakumfukuza bali alimwendea na kumtazama mtoto. Alipoiona hali ya mtoto hairidhishi aliamuru mtoto alazwe hospitalini bila kujali kama alikuwa na pesa au la (uk.3-5).

Daktari Siki pia amesawiriwa kama jasiri. Sifa hii inadhihirika kupitia tendo lake la ujasiri la kwenda nyumbani kwa Meya kumweleza hali za Wanacheneo kinaga ubaga. Kwa mfano:

**Siki:** (*Kwa upole*). Sikiliza Sosi. Hizi si habari za kugoma au kutogoma. La hasha! Ni habari za hali ya maisha ya watu waliokuchagua wewe kwa kuamini kuwa utaziboresha hali zao. Watu wanakulilia. Wanataka uwasikilize. Hali yao ya maisha ni ngumu. Wanashindwa kumudu gharama za matibabu na kupanda na mahitaji nayo yanazidi kuongezeka ilhali mishahara haipandi…

**Meya:** Nd'o unamaanisha nini?

**Siki:** Kwamba hali si nzuri. (uk.10-11)

Kupitia dondoo hii tunaona ujasiri wa daktari Siki wa kuweza kumweleza Meya waziwazi juu ya vilio vya watu wake bila uoga. Daktari Siki pia ni mshauri. Sifa hii inadhihirika kupitia tendo lake la kumwendea Meya kumshauri juu ya uongozi bora, anasema:

**Siki:** Bwana Meya, mimi ninakwambia kama ndugu yako. Sisemi kwa sababu ya siasa. La! Ukweli ni kwamba watu wetu wana tatizo. Watu wetu wana tatizo. Watu wetu wana njaa. Wana kiu ambayo haikuzimwa. Ni hatari kuwaongoza watu wenye kukosa haya mawili. Huenda isichukue muda mrefu… (uk.12)

Kupitia dondoo hii daktari anampa Meya ushauri mzuri. Meya angelimsikiliza daktari Siki, mgomo wa wafanya kazi na kukamatwa kwake hakungelitokea.

Vilevile vitendo vya Gedi (vya mazoea) vya kwenda mbio kila anapoitwa na Meya, kusimama wima na kupiga saluti kila wakati anapokuwa mbele ya Meya vinatufanya tumuone kama mtumishi mnyenyekevu na mtiifu kwa bwana wake. Pia tabia yake ya kuitikia '*yes sir'* kila anapoitwa na Meya pia ni ishara ya utiifu.

#### 4.1.2.1.2 Tendo la kukwepa

Hili ni tendo ambalo mhusika anapaswa kulitenda lakini halitendi. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* tendo la Sele la kukataa kuwala vidagaaa, linamsawiri kama mhusika mwenye huruma. Sifa hii imedhihirika kupitia mazungumzo ya Zainabu na Bi. Rahma kama ifuatavyo:

**Bi. Rahma:** Hata Vidagaa si vibaya.

**Zainabu:** Hivyo ndo hali kabisa basi. Anavichukia.

**Bi. Rahma:** Havipendi?

**Zainabu:** Anasema anavipenda sana….

**Bi. Rahma:** Basi mpikie hivyo na sima. Si chapati na wali tu mwanangu!

**Zainabu:** Shangazi, Sele ana tabia za ajabu sana siku hizi kama nilivyokueleza. Anasema eti anawaonea dagaa huruma kuliwa na papa na yeye pia awale. (*Kimya*) Anasema huku ni kuonewa maradufu. Anasema anasema…eti tena kuwa hapendi vinavyoliwa huku vinatazama tu. (uk. 15-16).

Kupitia dondoo hii tunaona kuwa Sele anakwepa kula vidagaa, kwa kuwa anawaonea huruma kwa kuliwa na papa naye awale vilevile. Pia kupita tendo hili Sele anaonekana kama mtetezi wa wanyonge. Kwa kusema ‘vinavyoliwa huku vinatazama’ inamaanisha vidagaa ni wanyonge hawawezi kujitetea. Hivyo basi anapinga tendo la papa la kuwala vidagaa; kwa kutokula vidagaa yeye mwenyewe.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kukosa kubaki hospitalini kwa nesi Waridi wakati mazingira ya kufanya kazi yalipokuwa magumu, ni ishara ya kukosa kuwajibika na kukata tamaa. Binamu yake alipofariki, nesi Waridi aliamua kuacha kazi badala ya kuvumilia pamoja na daktari ili kuwapa wagonjwa tumaini na kuungana na wenzake kutafuta suluhisho kwa matatizo ya wafanyakazi.

Tendo hili la nesi Waridi la kukwepa majukumu yake, linatufanya tumuone nesi Waridi kama mhusika asiyeweza kuvumilia dhiki. Kupitia kwake tunaona utu na uvumilivu wa daktari Siki.

#### 4.1.2.1.3 Tendo la Kunuia

Huu ni mpango wa anachonuia kukifanya mhusika. Tendo halijafanyika lakini mhusika anakusudia kulitenda. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mipango ya Madiwani yakutaka kuongezewa mishahara na kutotozwa kodi inadhihirika kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Diwani II:** | Kwa unyenyekevu Mstahiki Meya nakuomba uwakumbuke walinda usalama wa Cheneo. Waongeze mshahara au marupurupu ili wawe na moyo wa kufanya kazi kwa uzalendo… |
| **Diwani III:** | Ndugu zangu, hazina ya Baraza la Cheneo tayari haiwatoshelezi wafanyakazi wake. Kuna nakisi ya shilingi milioni mia moja ishirini. |
| **Meya:** | Hilo si neno. Tutatafuta namna ya kufidia nakisi hiyo. Walinda usalama wataongezwa asilimia shirini… (*Kwa mkazo*) Uchumi na kazi, lile ombi la kutaka wasitozwe kodi limekubaliwa na lianze kutekelezwa mara moja. Sawa? (*Kimya. Kwa ukali*). Waelewa? |
| **Diwani III:** | Ndugu Meya, kama nilivyosema, Baraza lina nakisi. Huku kutowatoza ndugu zetu kodi ni kuongeza nakisi ya Baraza. (*Kimya*) Iwapo mama muuza ndizi analipa kodi ili kuchangia kulijenga taifa, iweje kwamba madiwani wasilipe kodi? |
| **Meya:** | Ni uamuzi wa Baraza. Ni demokrasia hii. Wengi wape. |
| **Diwani III:** | (*Shingo upande*) Sawa. |
| **Meya:** | Hakikisha kuwa kuanzia mwezi huu mishahara yao haitozwi kodi. Tayari wana mzigo mkubwa wa kulihudumia baraza. |

**Diwani I:** Madiwani hawamudu kuvaa vizuri wala kupata kununua nguo nzuri na kuwa nadhifu kama wenzao katika mapokezi ya mameya wanaokuja kutoka ng'ambo. (uk.22-23)

Kupitia tendo hili, ubinafsi na ulafi wa Diwani I na II unadhihirika, wanajali maslahi yao tu ilhali watu wanakufa kwa njaa na ugonjwa. Vilevile sifa ya udikteta imedhihirika kwa Meya pale anatoa amri kwa Diwani III atekeleze matakwa ya Diwani I na II mara moja. Pia sifa ya Diwani III ya utetezi wa haki inadhihirika kwa kumtetea mama muuza ndizi kutozwa kodi ilhali madiwani wasitozwe kodi.

Tendo la Sele katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* la kutaka kufanyiwa '*plastic surgery*' linadhihirisha sifa yake ya kutoridhishwa na maumbile yake na nia yake ya kutaka kuyabadili. Hili limedhihirika katika kurasa 31-36. Hali hii ya Sele inawakilisha mataifa ya Kiafrika yasiyoridhishwa na hali zao na kutaka kuiga mataifa ya ng'ambo.

#### 4.1.2.2 Usemi

Usemi wa mhusika ama katika mazungumzo au fikira zake akilini zinaweza kutumika kama mojawapo ya mbinu za kumsawiri mhusika. Katika usemi, tunaangalia mambo mawili:

i. Namna mhusika anavyoongea.
ii. Mazungumzo ya mhusika ama kujihusu au kumhusu mhusika mwingine.

##### 4.1.2.2.1 Namna Mhusika Anavyoongea

Kupitia namna mhusika anavyozungumza pia tunaweza kupata wasifu wa mhusika huyo. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kwa kutazama namna anavyowaongelesha Dida na daktari Siki (uk.9-14) sifa ya Meya ya ukali, mamlaka na dharau inadhihirika. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| **Meya:** | Dida! |
| **Dida:** | (*Kwa upole*.) Mstahiki Meya. |
| **Meya:** | (*Kwa ukali*.) Hivi una nini? |
| **Dida:** | (*Anashangaa. Anajibu kwa upole.*) |
| | Mstahiki Meya lipo lililoenda Kombo? Samahani sana… |
| **Meya:** | Sina haja ya hadithi zako za pole. Amekutuma nani kunichoma kwa chai mapema hii? Una njama gani? (uk.9) |

Kupitia namna wahusika hao wawili, Meya na Dida wanavyozungumza tunaweza kutathmini tabia zao. Meya anadhihirika kama mkali na mwenye mamlaka dhidi ya Dida. Dida naye anadhihirika kama mpole na mnyenyekevu mbele ya Meya. Hii ni kupitia namna anavyoongea kwa upole na kwa kutumia jina la heshima 'mstahiki Meya' anapomrejelea Meya. Dharau ya Meya inadhihirika kwa namna anavyoongea na daktari Siki. Anasema, "(*Kwa dharau*.) Hivi unaona kuwa uongozi wangu hautaenda mbali?" (uk.12). Hapa tunaona namna Meya anavyoongea kwa dharau. Hivyo basi ni mwenye dharau.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* Sele amesawiriwa kama mwenye hasira na asiyependa kusumbuliwa. Haya yamedhihirika kupitia namna anavyoongea kwa ukali kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Sele:** | (*Kwa sauti ya juu.*) Wewe umejua kama mimi sitaki mtu kunisumbua halafu unanijia kwa fujo. Dharau tu! (uk.33) |

Hii ni dhahiri kuwa Sele ana hasira za haraka na hapendi kusumbuliwa. Kuingia kwa Aisha chumbani alimokuwemo bila kubisha kulimghadhabisha sana Sele hadi akaongea kwa ukali.

Vilevile kupitia matumizi ya lugha, tunaweza kuthamini kiwango cha elimu, tabaka na mazingira ya mhusika. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, Jamila anavyoongea

kunaashiria tabaka na kiwango chake cha elimu na anaweza kutafautishwa na wahusika wengine kama vile Aisha, Sele, Bi. Rahma, Zainabu, Musa na Amin. Jamila anatumia jagoni za kimatibabu anapoongea na Bi Rahma na Zainabu. Kwa mfano, anasema,

> **Jamila:** Ulikuwepo lakini si sana. Unajulikana katika lugha ya utabibu kama *Body Dysmorphic Disorder,* yaani B.D.D (*kimya*). Ni hali ya mtu kujikuta kutoipenda sehemu fulani ya mwili wake na kuichukia… (uk.90)

Kupitia usemi huu, Jamila anadhihirika kama msomi na kupitia maelezo yake tunaweza hatimaye kuufahamu ugonjwa wa Sele.

Katika tamthilia *Mstahiki Meya*, kwa mfano tunamuona Dida akitumia msamiati kama vile 'Mstahiki Meya', 'Mstahiki baba Meya' na 'baba' (uk.9). Dida anatumia msamiati huo anapoongea na Meya. Hii inadhihirisha tabia ya unyenyekevu na heshima ya Dida. Vilevile tunapata kuona ni nani mwenye mamlaka kati ya Dida na Meya. Mamlaka ya Meya dhidi ya Dida yanadhihirika kupitia msamiati wanaotumia katika mazungumzo yao kama ifuatavyo:

> **Meya:** Dida!
>
> **Dida:** (*Kwa upole*) Mstahiki Meya! (uk.9)

Kupitia mfano huo, tunamuona Meya akimwita Dida kwa jina lake ilhali Dida hathubutu kumuita Meya kwa jina lake. Dida anatumia msamiati wa heshima.

Aisha katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* amejitokeza kama mwenye heshima kwa wazee wake. Hili linadhihirika pale anapoongea na Bi. Rahma hamuiti kwa jina laka kama vile anavyomuita mumewe; Sele. Kwa mfano anapomuamkia anasema, "Bibi shikamoo*!*" (uk.18). Pia anapoongea na Musa anamuita 'baba' (uk.47). Uteuzi huu wa msamiati wa heshima ndio unaomsawiri Aisha kama msichana mwenye heshima.

Mhusika Amri katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* amesawiriwa kama mwenye busara. Busara yake inadhihirika kupitia matumizi ya misemo na mafumbo katika mazungumzo yake. (uk.64-70)

#### 4.1.2.2.2 Mazungumzo ya Mhusika

Tabia ya mhusika inaweza kutathminiwa kupitia anayoyasema ama kujihusu au kumhusu mhusika mwengine. Mazungumzo haya yanaweza kuainishwa katika aina mbili: kwanza, Mhusika na wasifu wake na pili, mhusika na wasifu wa mhusika mwengine.

##### 4.1.2.2.2.1 Mhusika na wasifu wake

Kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kupitia anayoyasema Meya yanaashiria ufisadi wake.

> **Meya:** … Mimi nimeuza vipande vyangu vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii. Nimebakiza vitano *incase*. Wewe nilikugawia vinne. Unaweza kuuza kimoja au viwili kwa ajili hiyo. Vingine viweke kwa ajili yao hao watoto unaowahangaikia, hasa ile *prime plot*. (uk. 27)

Kupitia usemi huo wa Meya tunaweza kusema kuwa ni fisadi. Amenyakua vipande vinane vya ardhi vya umma na hata kumzawadi Bili vipande vinne vya ardhi. Vilevile Meya amejitokeza kama msaliti pale anaposema:

> **Meya:** Ndiyo maana alisafiri ng'ambo. Madaktari wetu hawa wa kubabaisha tu. Kule ng'ambo ndipo walipo wakunga wenyewe. Sikutaka kubahatisha. Halafu tena mtoto akizaliwa huko anapata uraia wa huko huko. (uk. 27)

Usemi huu unaonyesha ukosefu wa uzalendo na usaliti wa Meya. Kama kiongozi angekuwa mfano mwema wa kuigwa. Badala ya kuboresha huduma za afya katika

eneo lake anapendelea kupeleka familia yake ng'ambo kwa matibabu tena kwa pesa alizopata baada ya kuuza vipande vya ardhi alivyonyakua. Pia anataka mtoto wake akizaliwa apate uraia wa ng'ambo.

Kupitia usemi, tabia za wahusika mbalimbali zimedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. Kwa mfano, kujichukia kwa Sele kunadhihirika kupitia usemi wake. Anasema:

**Sele:** Ni kama nilivyokuambia. Sipendi hili kovu.
Uso kwa jumla. Vyote hivi vinasumbua moyo wangu. Lakini langu ni hili moja! Sipendi mkao wa uso wangu. Ninauchukia, unanikera. Sipendi pua hii. (*Anaashiria*)
Pua mbaya hii… (uk.33-34)

Kupitia usemi huu inadhihirika jinsi Sele anavyochukia maumbile yake. Hivyo kumfanya kujichukia. Chuki hii ndiyo chanzo cha ndwele yake na ndicho kijiba chake cha moyo. Chuki hii ya Sele inaashiria jinsi mataifa yanayoendelea yanavyokosa kujithamini.

**4.1.2.2.2.2 Mhusika na wasifu wa mhusika mwengine**

Mhusika na wasifu wa mhusika mwengine unadhihirika Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kupitia usemi wa Dida anasema:

**Dida:** Kuna roho ya mtu na ya kiatu
Na hizi mbili ni tofauti
Meya anajua hili
Watu wake wana roho za watu
Naye hakusita mbali akazipeleka
Mbali na urundo na joto la jiji
Katika salama ya utulivu wa mandhari.
(uk. 65)

Usemi huu wa Dida unashadidia usaliti, ukosefu wa uzalendo, na ubinafsi wa Meya. Meya anajali maslahi ya familia yake pekee. Ameipeleka familia yake mbali na uvundo unaotokana na mlimbiko wa taka na joto la maandamano ya wafanyakazi wa baraza la Cheneo.

#### 4.1.2.3 Muonekano wa Nje

Mhusika anaweza kusawiriwa kupitia anavyoonekana ama kupitia maumbile yake au mtindo wake wa mavazi na mitindo ya nywele.

##### 4.1.2.3.1 Maumbile

Mbinu hii ya usawiri imedhihikika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* kupitia usemi wa Aisha. Anasema:

> **Aisha:** "Haukukai vizuri? (*Anamkaribia na kumtazama*) Mimi naona uso mzuri wenye pua nzuri iliyochongeka vizuri. Tena yenyewe laini. (uk.33)

Kupitia usemi huu wa Aisha tunapata taswira ya maumbile ya uso wa Sele. Hivyo basi kuweza kumbainisha miongoni mwa wahusika wengine. Tunapata kujua kwamba ana uso mzuri wa kupendeza wenye pua laini na iliyochongeka vizuri.

Maumbile ya Sele pia yamesimuliwa kupitia usemi wake mwenyewe anaposema, "Mlinicheka kwa mwendo wangu wa mataga mataga. Mlinicheka kwa midomo yangu mikubwa. Nilichekwa kwa weusi uliokoza na kukolea…" (uk.43)

Kupitia usemi wa Aisha na usemi wa Sele, tunapata taswira kamili ya maumbile ya Sele. Kutokana na maelezo hayo tunaweza kumuona Sele kama kijana mwenye sura ya kupendeza yenye pua laini iliyochongeka vizuri na midomo mikubwa. Vilevile ana mataga na weusi uliokoza na kukolea.

Maumbile haya ndiyo yanayokuwa 'kijiba cha moyo' kwa Sele. Sele anachukizwa na maumbile yake, hana utulivu moyoni. Anashinda mbele ya kioo akijitazama uso na hatimaye anaamua kufanyiwa '*plastic surgery*'. (uk.31-36). Dhana hii ya Sele kutothamini uzuri wake inawakilisha mataifa ya Kiafrika yanayoendela ambayo hayajiamini kwa utajiri wa raslimali na uwezo yaliyonayo na hivyo basi kutaka kujifafanisha na mataifa yaliyoendelea.

#### 4.1.2.3.2 Mavazi

Kupitia mavazi ya mhusika pia tunaweza kupata wasifu wa mhusika. Kwa mfano katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* Sele na daktari wamesawiriwa kwa kutumia mavazi yao kama ifuatavyo:

> Hospitalini. Inakaribia magharibi. Sele amevalia sare za wagonjwa…Daktari katika mzunguko wake wa kuwatembelea wagonjwa anaingia kwa kasi huku amevaa sare za kazi na glavu za mkono. (uk.52)

Katika dondoo hii kupitia mavazi ya wahusika tunaweza kutathmini wasifu wao. Sele ni mgonjwa kutokana na mavazi ya wagonjwa aliyovaa na daktari si mgonjwa bali ni daktari kwa sababu amevaa sare za kazi na glovu tayari kutibu wagonjwa.

Usawiri wa aina hii pia umejitokeza katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Kwa kupitia mavazi, daktari Siki amesawiriwa kama ifuatavyo:

> Jioni. Zahanati. Daktari Siki katika mavazi yake rasmi anaonekana mwenye wasiwasi… (uk.1)

Mavazi 'rasmi' ya daktari yameelezewa zaidi katika hadithi ambapo tunaelezwa:

> Katika ofisi ya Siki. Siki ameketi akisoma gazeti kuna <u>koti jeupe la kazi</u> lililokunjwa vizuri kando ya meza. (uk.34)

> ……………………………………………………………...
>
> Tatu anaondoka. Siki anabaki ofisini. Analichukua koti lake jeupe, analikunjua na kulitundika kwenye msumari ukutani. (uk.40)

Kutokana na maelezo yote haya tunapata picha kamili ya mavazi ya daktari Siki. Ambapo tunaelezwa anavalia koti jeupe. Kupitia kuvaa koti jeupe tunaweza hata kumtofautisha na mwanasiasa. Meya ambaye mavazi yake ni suti. Mavazi ya Meya yanadhihirika pale alipomwagikiwa na chai. Tunaelezwa:

> **Dida:** (*Anagundua kuna chai iliyomwagikia kiti na meza.*) Samahani sana Mstahiki baba Meya. Nimeitoa chai chupani kama kawaida (*Huku akipangusa samani na koti la Meya.*)

Kupitia dondoo hii tunamuona Meya akiwa amevalia koti akijiandaa kwenda ofisini. Hii inaashiria kuwa ni mtu wa hadhi ya juu akilinganishwa na daktari Siki anayevaa Sare za kazi (Koti jeupe) aendapo kazini.

#### 4.1.2.4 Mazingira

Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (1983), maeneo aliyomo mhusika (chumba, nyumba, barabara, mji) na vilevile mazingira ya kijamaa (familia, tabaka) hutumika mara nyingi kumsawiri mhusika. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mara ya kwanza kukutana na Meya; tunamuona nyumbani kwake.

> Siku ya pili asubuhi, nyumbani kwa Meya, Meya ameketi mezani mbele yake kuna mayai kadhaa katika sahani na kikombe cha chai. Pembeni kuna makochi ya kupendeza, sakafuni kuna zulia lenye ruwaza za kupendeza. Vilevile kuna vyakula vya aina mbalimbali mezani. (uk.8)

Mazingira aliyomo Meya ni nyumbani kwake sebuleni ambako kuna meza, makochi ya kupendeza na zulia lenye ruwaza za kupendeza. Mazingira hayo yanaashiria hali

ya utajiri. Pia tunaelezwa kuwa Meya ameketi mezani nambele yake kuna mayai kadhaa katika sahani na vyakula vya aina mbalimbali. Kuwepo kwa vyakula kochokocho kwa ajili ya mtu mmoja tu inaashiria ulafi na ubadirifu wa Meya. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa Meya ni tajiri na mbadirifu.

Kwa upande wa mazingira ya kijamaa, Meya ana familia. Hii inadhihirika kupitia mazungumzo yake na Bili kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Bili:** | Ndivyo hivyo. Je, habari za watoto na mama yao? |
| **Meya:** | Wamekuwa na mafua kidogo lakini sasa yanapungua. Mama yao jana amenipigia simu akanieleza kwamba wanaendelea vizuri. |
| **Bili:** | Mafua ni jambo la kawaida. Wanasema ni ya pua tu. Mama anakupigia simu kutoka wapi tena? Au amesafiri kwenda nyumbani! |
| **Meya:** | Hata kidogo. Amekwenda ng'ambo kuwaona watoto wake. Siku ile nilikwambia hawasomei hapa tena. Viwango viko chini kidogo. (uk.26) |

Kupitia mazungumzo haya tunapata kujua kuwa Meya ana mke na watoto ingawa watoto wake amewapeleka ng'ambo kusoma. Hili linadhihirisha usaliti wa Meya kwa nchi yake. Hana uzalendo, anathamini elimu ya ng'ambo kuliko katika nchi yake.

Mbinu hii ya usawiri wa wahusika pia imedhihirika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. Wakati mwingi Sele amesawiriwa akiwa katika mazingira ya nyumbani kwake haswa chumbani mwake. Katika hadithi nzima Sele alitoka mara moja tu, alipoenda hospitalini (uk.52-62) kisha baada ya kutoka hospitalini alienda moja kwa moja kwa babu yake, Amri (uk.63-70). Huku kukaa ndani ndiko kunakoashiria ugonjwa wa Sele.

Katika mazingira ya kijamaa, tunamuona, Sele amezungukwa na familia yake akiwemo baba, mama, bibi, babu na mke wake. Jamaa wote wa Sele wanamhangaikia kutafuta tiba kwa ugonjwa wake. Sele anajitokeza kuwa mkaidi. Hakubaliani na kila analoambiwa na jamaa zake wala daktari kuhusu ugonjwa wake. Anakaidi kula chakula na hata kumeza dawa.

#### 4.1.2.5 Analojia

Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (1983), mbinu ya analojia inaweza kutumika kushadidia tabia ya mhusika na wala sio aina ya kivyake ya kuwasawiri wahusika. Katika analojia kuna matumizi ya sitiari. Kuna mfananisho wa majina ya majazina ulinganuzi wa wahusika.

##### 4.1.2.5.1 Majazi

Rimmon-Kenan (1983) akiwanukuu Hamon (1972) na Ewen (1980) anasema, kulingana na Hamon (1972) majina yanaweza kufanana na sifa za mhusika kwa namna nne; jina linavyoonekana, linavyosikika, linavyotamkwa na umbo lake. Naye Ewen (1980) anaeleza kuwa kuna uhusiano wa kisemantiki baina ya jina na tabia ya mhusika. Uhusiano huu wa kisemantiki ndio unaodhihirika katika tamthilia ya *Mstahiki wa Meya*.

Kwa mfano, jina Waridi alilopewa nesi ni la kimajazi. Waridi ni ua lenye miiba mikali na huchanua na kunawiri wakati wa alasiri na hunyauka na kupukutika wakati wa jua kali. Kama lilivyo jina lake, nesi Waridi 'miiba' (ukali) wake unaodhihirika pale ambapo anamrudi mama ambaye alipuuza foleni na kujitokeza ahudumiwe mbele ya wagonjwa wengine waliofika hospitalini mapema. Vilevile, hali inapozidi kuwa ngumu na kuzorota hospitalini nesi waridi anajiuzulu na kuacha kazi.

Siki ni jina la mhusika ambaye ni daktari. Kulingana na kamusi ya (TUKI 2014) Siki ni maji ya matunda yaliyochachuliwa kwa makusudi ambayo hutumika kuongezea ladha katika baadhi ya vyakula au dawa. 'Uchachu' wake daktari Siki unamuudhi sana Meya ambaye hataki kuambiwa ukweli kuwa umma unateseka. Hata hivyo,

upande wa wafanyakazi unanufaika kwa mchango na ushauri wake; aliweza kuhamasisha harakati za kupigania haki za wafanyakazi kupitia kiongozi wao; Tatu. (uk.39)

Jina Kheri alilopewa Diwani III ni la kimajazi kwani ni diwani mwenye kujali maslahi ya wanyonge na anawapigania dhidi ya viongozi wenye tamaa na ubinafsi mwingi. Kulingana na kamusi ya (TUKI 2014) jina kheri linamaanisha neema, baraka, ustawi na fanaka.

Bili ni jina alilopewa rafiki na mshauri wa Meya. Kulingana na kamusi ya (TUKI 2014) bili ni orodha ya huduma inayotolewa ya vitu vilivyouzwa pamoja na kiasi cha fedha zinazodaiwa; ankara. Kupitia ushauri wa mhusika huyu baraza linapata hasara kubwa kwa kulipia gharama ambazo hazifai kama nyongeza za mishahara ya madiwani, marupurupu, fidia kwa mwanakandarasi na hongo kwa mhubiri. Amegawiwa vipande vya ardhi vya umma na Meya kama mshauri wake na pia ndiye aliyezua wazo la kuuza fimbo ya Meya.

#### 4.1.2.5.2 Ulinganuzi wa Wahusika

Hii ni njia ambapo wahusika wawili wanawekwa katika muktadha sawa, usawa au tofauti katika tabia zao ndizo zinazoshadidia sifa au wasifu wao. Ulinganuzi unajulikana kama kulinganisha kwa kinyume.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, kwa mfano tunamuona Zainabu (mamake Sele) anavyokosa utulivu kwa sababu ya ugonjwa wa Sele, anaizungumzia hali hii mara kwa mara, ilhali Musa (babake Sele) anaonekana mwenye utulivu na asiyeshtushwa sana na ugonjwa wa Sele. Zainabu anataka kufanya uamuzi juu ya matibabu ya Sele hata bila kumshauri mwenyewe. Lakini Musa anaonelea kabla ya kufanya uamuzi wowote lazima Sele mwenyewe ahusishwe kwani ni mtu mzima. Zainabu anamuona Sele kama kwamba bado ni mtoto.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, tumeweza kuwalinganua daktari Siki na nesi Waridi. Wote ni wauguzi katika zahanati ya umma. Hali inapozidi kuwa mbaya hospitalini, nesi Waridi anaamua kuacha kazi hali hii inatupelekea kumuona waridi kama mtu asiye na stahamala na mwenye ubinafsi. Daktari Siki anabaki akiwapa wagonjwa matumaini, hivyo basi ni mvumilivu na mwajibikaji katika kazi yake.

**Hitimisho**

Sura hii imejadili usawiri wa wahusika katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Utafiti huu umebainisha kuwa mbinu zote mbili za usawiri wa wahusika, usawiri bainishi na usawiri timbe umedhihirika kwa wingi katika tamthilia zote mbili. Vilevile matumizi ya majina ya majazi yametumika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Ulinganuzi wa wahusika umetumika kushadidia wasifu wa wahusika katika tamthilia zote mbili. Kupitia usawiri wa wahusika umetuwezesha kuzielewa sifa za wahusika na hivyo basi kutupelekea kufahamu dhamira na maudhui katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*.

# SURA YA TANO

## MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 UTANGULIZI

Katika tasnifu hii tumeshughulikia usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kutathmini usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* na ulinuia kubainisha vipengele vya usimulizi na dhima ya vipengele hivyo katika usimulizi wa hadithi kwenye tamthilia zilizokuwa zinachunguzwa.

Vipengele vilivyochunguzwa ni pamoja na kipengele cha wakati, daraja na sauti za usimulizi na wahusika na uhusika. Tumegundua kuwa dhana ya usimulizi ni pana mno. Vilevile tumegundua kuwa tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* zimefumbata kwa kiasi kikubwa vipengele vya usimulizi vilivyokuwa vinachunguzwa na utafiti huu.

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo na kufafanua iwapo malengo yetu yaliafikiwa au la. Vilevile kutoa mapendekezo kuhusu tafiti zijazo kuhusu suala la usimulizi katika tamthilia kwa jumla.

### 5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Katika sura ya kwanza tulibainisha nadharia tete mbili ambazo utafiti huu ulinuia kuchanganua. Kutokana na utafiti wetu tunaweza kusema kwamba nadharia tete zetu zimethibitika. Awali tulichukulia kwamba usimulizi hauna nafasi muhimu katika tamthilia. Kutokana na utafiti huu tumebainisha kwa kutumia mifano na data kutoka katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya* kuwa vipengele vya usimulizi vimo katika tamthilia hizo mbili na vina umuhimu mkubwa katika kusimulia hadithi na kupitisha maudhui na dhamira za kazi hizo, kwa mfano katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, kupitia usawiri wa Meya, maudhui kama vile uongozi mbaya, usaliti, unafiki miongoni mwa viongozi yameweza kupitishwa.

Katika sura ya pili, kazi hii imeangazia kipengele cha wakati na mihimili yake. Imebainika kuwa tamthilia zote mbili zina matumizi ya analepsia na prolepsia. Analepsia zimetumika kusimulia matukio yaliyotokea kabla ya wakati wa 'sasa' wa hadithi. Kupitia analepsia tuliweza kufahamu matukio yaliyopita. Prolepsia zimetumika katika tamthilia zote mbili ingawaje sio kwa wingi kama vile analepsia. Kupitia prolepsia tuliweza kufahamu matukio kabla ya wakati wake wa kutokea.

Muda umeweza kudhihirika kupitia matumizi ya muhtasari, mtuo, onyesho na udondoshi katika tamthilia zote mbili. Muhtasari haukubainika kwa wingi. Mtuo umedhihirika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* kupitia masimulizi ya msimulizi wa daraja ya kwanza. Onyesho ndilo lililotawala kazi zote mbili ambako tumepata mazungumzo baina ya wahusika. Udondoshi bayana, udondoshi uso kikomo, udondoshi dhahiri na udondoshi batini wote umedhihirika katika tamthilia zote mbili. Kupitia udondoshi, kasi ya usimulizi iliweza kudhihirika. Tamthilia zote mbili pia zimedhihirisha matumizi ya usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu.

Sura ya tatu imeangazia daraja na sauti za usimulizi. Imebainika kwamba tamthilia zote mbili zina hadithi ya daraja ya kwanza, daraja ya pili na daraja ya tatu mtawalia. Daraja ya tatu ni hadithi tegemezi ambazo zimeegemezwa katika daraja ya pili. Hadithi hizi tegemezi zimekuwa na dhima mbalimbali katika usimulizi, kama vile dhima ya kiutekelezi, kiufafanuzi na kimaudhui.

Tamthilia zote mbili zimetumia usimulizi tangulizi, usimulizi wa kiurejeshi na usimulizi sawia. Hata hivyo usimulizi uliotumika kwa kiasi kikubwa ni ule usimulizi sawia. Kupitia usimulizi sawia matendo ya wahusika yaliweza kusimuliwa sambamba na yanavyotokea.

Aina za wasimulizi na wasimuliwa zimeangaziwa katika sura hii. Imedhihirika kuwa katika tamthilia zote mbili kuna wasimulizi tawasifu, wasifu, wasimulizi wa daraja ya kwanza na daraja ya pili pamoja na wasimulizi wazi. Kupitia wasimulizi wa daraja ya

kwanza, usimulizi wa hadithi msingi umefanyika. Aina hizi mbalimbali za wasimulizi zimechangia kuwepo na usimulizi kupitia mitazamo mbalimbali.

Hivyo basi tunaweza kusema kuwa usimulizi katika tamthilia zote mbili ni changamani. Tumeweza kupata usimulizi wa aina tatu, nazo ni usimulizi ngazi ambapo kuna hadithi inayotegemezwa kwenye hadithi kuu. Usimulizi maizi ambapo msimulizi ana ufahamu wa kila kitu kinachotokea katika hadithi na usimulizi penyezi ambapo mwandishi anajitokeza mara kwa mara kutoa maoni, tathmini au mapendekezo. Wasimuliwa ambao wamedhihirika katika tamthilia hizi ni wasimuliwa wa daraja ya kwanza na pili. Pia wasimuliwa wamebainishwa wazi ingawa kwingine sio wazi.

Sura ya nne imepambanua wasifu wa wahusika kupitia uhusika. Katika uchunguzi huu wa wahusika na uhusika imedhihirika kwamba tamthilia zote mbili zimetumia aina mbili za usawiri wa wahusika kama zilivyopendekezwa na Rimmon-Kenan (1983). Nazo ni usawiri bainishi na usawiri timbe. Hata hivyo imebainika kuwa usawiri timbe ndio unaosheheni katika tamthilia zote mbili. Katika usawiri timbe Arege amefanikiwa kusawiri wahusika wake kupitia matendo, usemi, muonekano wa nje na mazingira. Vilevile ameweza kutumia analojia kushadidia tabia za wahusika, kama vile matumizi ya majina ya majazi na ulinganuzi wa wahusika. Usawiri wa wahusika umetuwezesha kuzielewa sifa za wahusika na hivyo basi kupelekea kufahamu dhamira na maudhui ya tamthilia zote mbili.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa tamthilia hizi mbili, *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*, zimetumia vipengele vya usimulizi vya wakati, daraja na sauti za usimulizi na wahusika na uhusika. Tumegundua kuwa vipengele hivyo vina umuhimu mkubwa katika usimulizi wa hadithi katika tamthilia hizo. Kwa hivyo, ni kweli kuwa vipengele vya usimulizi vinavyohusishwa na kazi za nathari vinaweza kupatikana katika tamthilia. Ni dhahiri kuwa vipengele vya usimulizi vinavyohusishwa na kazi za nathari vinaweza kupatikana katika tamthilia za Kiswahili, na vina dhima muhimu katika usimulizi wa hadithi katika tamthilia.

### 5.3 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya uchunguzi huu, tumegundua kuwa usimulizi ni mpana na kuna mengi ambayo yanaweza kutafitiwa katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Utafiti huu umeangazia vipengele vichache vya usimulizi. Kwa kuwa utafiti haungeweza kuchunguza vipengele vyote, tungependekeza tafiti za baadaye zichunguze vipengele vingine vya usimulizi ambavyo havijashughulikiwa katika utafiti huu.

Tafiti za baadaye zinaweza kuchunguza vipengele vyengine vya usimulizi kama vile mtazamo na usemi na hata vile ambavyo vimechunguzwa katika utafiti huu kwa upana na kina zaidi. Vilevile tungependekeza utafiti zaidi juu ya usimulizi katika tamthilia nyinginezo za Kiswahili kwa kutumia nadharia ya naratolojia kwa mitazamo tofauti.

## MAREJELEO


Arege, T. (2012) "Narration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi wa *Rasi'lGhuli*." Tasnifu ya PhD. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

_______ (2009) *Kijiba cha Moyo*. Nairobi: Longhorn Publishers.

_______ (2009) *Mstahiki Meya*. Nairobi. Vide~Muwa Publishers.

Bal, M. (1997) *Narratology Introduction to the Theory of Narrative* ($2^{nd}$Edition). Canada: University of Toronto Press.

De Villiers, G (2005) *A Narratological Analysis of the Babylonian Gilgamesh Epic According to the Model of G. Genette* 1980. University of Pretoria etd. Imesomwa (13/04/2015 7:04pm).http://repository.up.ac.za/bitstream/handle/2263/22989/05chapter5.pdf?sequence=6

Genette, G. (1972) *Narratology*. Imesomwa (Jumapili 08/03/2015 saa 2:00pm). http://www.signosemio.com/genette/narratology.asp

___________ (1980) *Narrative Discourse*. Ithaca: Cornell University Press.

Hussein, E. (1971) *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.

Kaui, T. (2012) *Mwongozo wa Mstahiki Meya*. Nairobi: Queenex Publishers.

Kimani, P. (2012) "Arki za Simulizi Katika Utendi wa *Mikidadi na Mayasa*." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

King'ei, G. etal (2012) *Mwongozo wa Mstahiki Meya* (Timothy M. Arege). Nairobi: Target Publishers.

Mbuthia, E (2012) *Mwongozo Changanuzi wa Mstahiki Meya*. Nairobi: Target Publishers.

Mbuvi, F. & Were, E. (2012) *Mwongozo wa Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Mohammed, S.A. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Muhando, P. (1962) *Hatia*. Nairobi: East Africa Publishing House.

___________ (1982) *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

____________ (1984) *Lina Ubani*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Mutegi, M. (1985) "Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthilia tano za Ebrahim Hussein." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Muturi, M. (2012) *Mwongozo wa Mstahiki Meya* (Timothy Arege). Nairobi: Top Achievers Publishers.

Mtobwa, B. (2004) *Mtambo wa Mauti*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Ndege, C. (2013) "Ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za Arege: Mtazamo wa Muundo." Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Okwena, S. (2013) "Matumizi ya Jazanda katika Tamthili Tatu za Timothy Arege." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ong'ondi, E. (2005) "Usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Oxford Advanced Learner's Dictionaries 8th Edn. (2010) Oxford: Oxford University Press.

Rimmon-Kenan, S. (1983) *Narrative Fiction Contemporary Poetics*. London: Routledge.

TATAKI (2014) Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Tatu. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Oxford University Press.

Wafula, R. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix publishers.

___________ (2003) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus publications.

___________ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus publications.

____________ (2008) *Kanzi ya Fasihi Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Were, E. (2012) "Fani katika Tamthilia ya Kiswahili: Uchanganuzi wa *Kiliocha Haki* (1981) na *Kijiba cha Moyo* (2009)." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).